# KUCHUNGUZA DHAMIRA ZA LUGHA YA UTANI KATIKA MASOKO YA KUUZIA SAMAKI KASKAZINI PEMBA

**SALIM KHAMIS ZUBEIR**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA KUTIMIZA MASHARTI YA KUTUNUKIWASHAHADA YA UMAHIRI YA KISWAHILI (M.A KISWAHILI) KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2023**

## UTHIBITISHO

Alietia saini hapa chini amethibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii, yenye mada isemayo: ***Kuchunguza Dhamira za lugha ya Utani katika Masoko ya kuuzia Samaki Kaskazini Pemba***. na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya masharti ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri ya Kiswahili (M.A Kiswahili) katika idara ya Lugha na taaluma za Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**…………………………………………….**

**DKT. Mohamed Omary Maguo**

**(Msimamizi)**

**Tarehe…………………………………**

**HAKIMILIKI**

Tasnifu hii ni mali yangu binafsi, hairuhusiwi kuihifadhi, kuibadili na kuiga kwa namna yoyote, kielektroniki, kurudufu nakala, kupigwa chapa, kuirikodi kwa utaratibu wowote, ila kwa ruhusa ya mwandishi wake au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## TAMKO

Mimi, **Salim Khamis Zubeir**, natamka na kuthibitisha kwamba hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na mtu yoyote katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyengine inayofanana na hii.

**……………………………………...…**

**Saini**

**…………………………….………**

**Tarehe**

## TABARUKU

Tasnifu hii ni zawadi njema kwa walimu wangu popote walipo duniani, marafiki na familia yangu kwa ujumla. Vileviletasnifu hii ni zawadi kwa marehemu bibi yangu Bi Mwanakhamis Nassor Hamad na marehemu babu yangu mpendwa Bw. Zubeir Ameir Hamad. Wote nawaombea kwa Mungu awalipe jazaa njema.Amiin.

## SHUKURANI

Naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu (S.W) mwingi wa rehma mwenye kurehemu,kwa kunijalia uzima usio na shaka na kunipa nguvu,uwezo juhudi maarifa na hekima kwa kufanikiwa kutekeleza na kukamilisha kazi hii muhimu.Vile vile natanguliza shukurani zangu za dhati kwa kipenzi cha waislamu wote Mtume Muhammad (S.A.W) na kumtakia rehma, neema na msamaha kwa Mwenyezi Mungu (S.W), Muumba wa Mbingu na Ardhi.

Aidha shukurani zangu za dhati ni kwa msimamizi wangu mpendwa Dkt. Mohamed Omary Maguo ambaye alidiriki kunisimamia vyema na kunipa muongozo bila kuchoka hadi kufikia hatma ya kazi hii ngumu iliyokuwa na changamoto nyingi na misukosuko hadi kukamilika kwake.Kati ya jambo zurina ambalo sitalisahau kutoka kwake ni uhodari wake,ukweli wake na juhudi zake kubwa ambazo alizionesha kwangu, kwani wakati wowote alikuwa tayari kuniongoza kwa kadri ya uwelewa wake.Bila ya juhudi zake kubwa alizozifanya kwangu ni dhahiri kazi hii isingalifanikiwa kwa kiwango hiki ambacho ni cha hali ya juu. Namuomba Mungu (S.W) Muumbawa Mbingu na Ardhi amlipe kila la kheri, amuepushie na balaa yeye na familia yake.

Vile vile nawashukuru walimu wangu Mw. Hemed Saidi Massoud, Mw. Amour Ali Rashid na Mwalimu Bakari Kombo Bakari wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania - Tawi la Pemba, (OUT) kwa kutusomesha vyema na kwa kutushajihisha, kutuhimiza na kutuongoza kwa kadri ya uwezo wao hadi kukamilika kwa tasnifu hii.

Shukurani nyengine ni kwa nduguzangu na jamaa wote walioweza kutoa mchango wao kwa njia moja au nyengine hadi kukamilika kwa tasnifu hii,miongoni mwao ni

mkuu wangu wa kazi,kutokana na ruhusa aliyokuwa akinipa mara kwa mara ili kufatilia uandishi wa tasnifu hii hadi kukamilika kwake. Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu wapenzi, miongoni mwao ni Haji Omari Kombo na Bimize Hamadi Juma, hawa walikuwa na mchango mkubwa hadi kukamilika kwa tasnifu hii.

Shukurani za pekee ni kwa wazazi wangu wapendwa, Bw. Khamisi Zubeir Ameir na Bibi, Maulida Rashidi Tani, pamoja na wake zangu Bi. Zainabu Mbaruk Moh’d na Bi Riziki Maalimu Sharif. Pia katika shukrani zangu siwezi kuwasahau watoto wangu ambao wao na mama zao kwa hakika waliniamini na kuonesha upendo na uvumilivu mkubwa kwangu. Nathubutu kusema kwamba bila ya uvumilivu wao ningalishindwa kukamilisha tasnifu hii.

## IKISIRI

Mada ya utafiti huu imehusu: *Kuchunguza dhamira za lugha za utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba.* Kwa mnasaba wa mada hii, utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi mawili: (i) Kuchambua dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba na (ii) Kubainisha mbinu za kisanaa za lugha za utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Data za utafiti zimekusanywa kwa kutumia mbinu za ushuhudiaji, usaili na upitiaji wa nyaraka na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na kushadadiwa na nadharia za Mwitiko wa Msomaji na Simiotiki. Matokeo ya yanaonesha kwamba, kwa upande wa dhamira zilizojitokeza katika utani wa masoko ya kuuzia samaki kisiwani Pemba ni kujenga umoja na mshikamano, kuelimisha jamii, kuburudisha jamii, ustahamilivu katika kazi, ujasiri, ukombozi, kuoyonya jamii na nyenginezo. Aidha, mbinu za kisanaa zilizobainika ni matumizi ya tashibiha, taswira, takiriri, ishara, kejeli, misemo, methali na tashtiti. Mwishoni mwa utafiti kumetolewa mapendekezo ya kufanya utafiti zaidi katika eneo la kipera cha utani ambacho kipo katika utanzu wa sanaa za maonesho ambacho ni muhimu kwa kukuza na kuendeleza utamaduni katika jamii mbali mbali.

**Maneno Muhimu:** *Utani, dhamira, mbinu za kisanaa*

# YALIYOMO

UTHIBITISHO ........................................................................................... ii

HAKIMILIKI ........................................................................................... iii

TAMKO ........................................................................................... iv

TABARUKU ........................................................................................... v

SHUKURANI ........................................................................................... vi

IKISIRI ........................................................................................... viii

YALIYOMO ........................................................................................... ix

ORODHA YA MAJADWELI ........................................................................................... xiv

ORODHA YA VIFUPISHO ........................................................................................... xv

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA ........................................... 1**

1.1 Utangulizi ........................................................................................... 1

1.2 Usuli wa Mada ........................................................................................... 1

1.3 Tatizo la Utafiti ........................................................................................... 4

1.4 Malengo ya Utafiti ........................................................................................... 5

1.4.1 Lengo kuu ........................................................................................... 5

1.4.2 Malengo Mahsusi ........................................................................................... 6

1.5 Maswali ya Utafiti ........................................................................................... 6

1.6 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................................... 6

1.6.1 Kwa Matumizi ya Nadharia ........................................................................................... 7

1.7 Mipaka ya Utafiti ........................................................................................... 7

1.8 Muundo wa Utafiti ........................................................................................... 8

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ............ 10**
2.1 Utangulizi ............ 10
2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu ............ 10
2.2.1 Maana ya Utani ............ 10
2.2.2 Maana ya Dhamira ............ 11
2.2.3 Maana ya Mbinu za Kisanaa ............ 12
2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizikuhusu Utani ............ 12
2.4 Pengo la Utafiti ............ 19
2.5 Mkabala wa Kinadharia ............ 20
2.6 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ............ 20
2.6.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ............ 21
2.6.2 Sababu ya Uteuzi wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ............ 22
2.6.3 Nadharia ya Simiotiki ............ 22
2.6.3.1 Misimbo ya Nadharia ya Simiotiki ............ 23
2.6.3.2 Sababu za Uteuzi wa Nadharia ya Simiotiki ............ 25
2.7 Hitimisho ............ 25

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ............ 26**
3.1 Utangulizi ............ 26
3.2 Eneo la Utafiti ............ 26
3.3 Usanifu wa Utafiti ............ 27
3.4 Kundi Lengwa ............ 28
3.5 Sampuli na Usampulishaji ............ 29

3.6 Ukusanyaji wa Data ............................................................ 30
3.6.1 Data za Msingi ............................................................ 30
3.6.2 Data za Upili ............................................................ 31
3.7 Mbinu za Kukusanyia Data ............................................................ 31
3.7.1 Mbinu ya Ushuhudiaji ............................................................ 32
3.7.2 Mbinu ya Usaili ............................................................ 32
3.7.3 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka ............................................................ 33
3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data za Utafiti ............................................................ 33
3.8 .1 Mbinu ya Mkabala wa Kimaelezo ............................................................ 34
3. 9 Maadili ya Utafiti ............................................................ 34
3.10 Hitimisho ............................................................ 35

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ............................................................ 36**

4.1 Utangulizi ............................................................ 36
4.2 Dhamira za Lugha ya Utani katika Masoko ya kuuzia Samaki Kaskazini Pemba ............................................................ 36
4.2.1 Dhamira ya Kujenga Umoja na Mshikamano ............................................................ 38
4.2.2 Dhamira ya Kuelimisha Jamii ............................................................ 39
4.2.3 Dhamira ya kuburudisha jamii ............................................................ 41
4.2.4 Dhamira ya ustahamilivu katika kazi ............................................................ 42
4.2.5 Dhamira ya kujenga ujasiri ............................................................ 43
4.2.6 Dhamira ya ukakamavu katika kazi ............................................................ 45
4.2.7 Dhamira ya kuhimiza jamii katika kazi ............................................................ 46

4.2. 8 Dhamira ya kuwa na upendo katika kazi ........................................................ 48
4.2.9 Dhamira ya kuonya jamii ................................................................................ 49
4.2.10 Dhamira ya mmong'onyoko wa maadili ......................................................... 50
4.2.11 Dhamira ya utamaduni katika jamii ............................................................... 51
4.2.12 Dhamira ya ukombozi ..................................................................................... 53
4.2.13 Dhamira ya Ukweli na Uwazi ......................................................................... 55
4.3 Mbinu za Kisanaa za Lugha ya Utani ............................................................... 56
4.3.1 Matumizi ya Tashibiha ...................................................................................... 57
4.3.2 Matumizi ya Taswira ........................................................................................ 58
4.3.3 Matumizi ya Takriri .......................................................................................... 59
4.3.4 Matumizi ya Ishara ............................................................................................ 59
4.3.5 Matumizi ya Kejeli ............................................................................................ 59
4.3.6 Matumizi ya Misemo ......................................................................................... 61
4.3.7 Matumizi ya majazi ........................................................................................... 64
4.3.8 Matumizi ya Methali .......................................................................................... 65
4.3.9 Matumizi ya tashititi .......................................................................................... 66
4.4 Hitimisho .............................................................................................................. 68

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........... 69**

5.1 Utangulizi ............................................................................................................. 69
5.2 Muhtasari ............................................................................................................. 69
5.3 Hitimisho .............................................................................................................. 70
5.4 Mapendekezo ....................................................................................................... 70
5.4.1 Mapendekezo kwa Jamii ................................................................................... 70

**MAREJELEO ........................................................................................................ 72**

**VIAMBATANISHO ................................................................................................ 78**

KIAMBATANISHO 1: MWONGOZO WA MASWALI YA UTAFITI KWA WATAFITIWA .................................................................... 78

KIAMBATANISHO II: JADWELI 02. MUHTASARI WA AINA ZA LUGHA YA UTANI KATIKA MASOKO YA KUUZIA SAMAKI KASKAZINI PEMBA........................................................ 80

KIAMBATANISHO III: ORODHA YA PICHA MBALIMBALI ZINAZOONYESHA KATIKA MASOKO YA KUUZIA SAMAKI KASKAZINI PEMBA....................................... 81

## ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli 01: Muhutasari waIdadi ya Watafitiwa katika Masoko ya kuuzia Samaki Kaskazini Pemba.................................................................. 27

Jedwali 02: Muhtasari wa aina za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ................................................................... 37

Jadweli 03: Muhtasari wa dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ................................................................... 56

Jadweli 04: Muhutasari wa mbinu za kisanaa za lugha ya utani........................... 67

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| A. S. W | Alaih Subuhana Wataala |
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili Zanzibar |
| Bi | Bibi |
| Bw | Bwana |
| Dkt | Dokta |
| Mw. Mungu | Mwenyezi Mungu |
| Mw. | Mwalimu |
| Nd. | Ndugu |
| n.k | nakadhalika |
| OUT | Open University of Tanzania |
| S.A.W. | Swalallah Alaihi Wasallama |
| S. W | Subuhanah Wataalah |
| SUZA | State University of Zanzibar |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Mada ya utafiti huu: *"Kuchunguza Dhamira za Lugha ya Utani katika Masoko ya kuuzia Samaki Kaskazini Pemba"*. Mtafiti amedhamiria kujadili vipengele muhimu katika sura hii, ikiwa ni pamoja na hivi vifuatavyo: Usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa utafiti.

## 1.2 Usuli wa Mada

Kwa mujibu wa TUKI (1990) Utani ni taratibu za kimila ambazo zinawafanya watu kuambiana au kutendeana jambo lolote bila ya chuki. BAKIZA (2010) inasema utani ni maneno au vitendo vya dhihaka au mzaha. Vile vile ikaendelea kusema kuwa utani ni tabia ya watu kufanyiana masihara kwa lengo la kuambiana kweli na kuimarisha uhusiano wao. Mtafiti wa kazi hii amejumisha mawazo ya makamusi haya mawili kwa kusema kwamba, ni uhusiano wa kijamii unaoruhusu watu kufanyiana dhihaka na kejeli pasina bughudha na chuki ndani yake. Aghalabu utani hulenga kufurahisha na kuchekesha na kuimarisha uhusiano baina ya wanajamii. Utani unaweza kujitokeza katika umbo la matendo, nyimbo, michoro au hadithi fupi fupi. Utani ni uhusiano wa jamii moja na nyengine kwa lengo la kuambiana kweli pasipo chuki kwa njia ya mzaha au dhihaka na zaidi utani hulenga kuchekesha au kufurahisha jamii. Sengo na Lucas (1975) wanaeleza kuwa utani ulianza kujitokeza tokea zama za kale na unaendelea hadi kufikia leo. Licha ya kuwa ni vigumu hasa kutambua utani ulianza lini na ulianza vipi, wapo wataalamu wanaoamini utani

ulianza mara baada ya mwanadamu kuanza shughuli zake za kazi. Pia wapo wataalamu wanaoamini utani ulileta na Waarabu.

Katika Afrika, utani unatumika kama sehemu ya burudani, lakini pia hutumika kwa kujenga uhusiano baina ya watu na kuimarisha udugu katika jamii. Udugu na uhusiano unaojengeka unakuwa mkubwa zaidi kuliko hata udugu wa damu. Kouyate (2003) kutoka Guinea ameeleza kuhusu dhana hii ya utani akasema kwamba, kwa kutumia utani mababu na mabibi huwalinda wajukuu zao kwa mnasaba wa kwamba wasiadhibiwe na wazazi wao kwa kile kinachoonekana ni kuwatia adabu. Kimsingi mambo yanayohusiana na hufungamana kwa kiasi kikubwa na mambo ya mila na desturi za jamii za watu. Matokeo ya utani hufanywa bila chuki baina ya watu wanaotaniana. Rashid (2018) akimnukuu Jones (2007) anbaye alisema kuwa, watu katika nchi ya Mali huutumia utani kwa kuuita *"Sinankuna"*. Sinankuna kimsingi inahusisha watu wenye historia na utamaduni wa aina moja na ambao wanaunganishwa na familia mbali mbali za kabila moja. Kwa mantiki hiyo ni wazi kwamba Sinankuna ni zaidi ya masihara, kwasababu inalenga kuepusha migogoro kwa mnasaba wa kulinda utamaduni.

Sengo na Lucas (wameshatajwa) wanasema mpaka hivi leo waandishi wengi wanakisia kwamba utani ulileta Tanzania na wafanyabiashara wa Kiarabu na hatimaye kuigwa katika mkondo wa taratibu za mwenendo wa Kibantu. Sengo (2009) anaeleza kuwa utani ni uhusiano wa kijamii uliojengeka baina ya pande mbili: Mosi, utani wenye lengo la kufurahisha, kufunza, na kukosowa. Pili, ni Utani wenye lengo la kukuza uhusiano kwa kuzingatia mila na desturi za watu husika. Ni kielelezo kimoja wapo kinachotambulisha mila na desturi katika jamii. Hata hivyo

utani unatafautiana kwa namna moja au nyengine, kulingana na tamaduni na jadi za watu kutoka jamii moja hadi nyengine.

Kwa mujibu wa Sengo na Lucas (1975), utani wa Kiafrika ni udugu mzito wenye chanzo chake kwenye matukio ya kimaisha. Wao wameuhusisha utani na matukio ya vita, njaa na matambiko. Kwa mujibu ya wataalamu hao, utani hubainika kama wa kifamilia kati ya babu na wajukuu zake, mume au mke na shemegi zake, utani kati ya mabinaamu, watoto wa shangazi na mjomba. Kwa ujumla, utani ni vitendo vya watu kufanyiana mzaha, masihara, dhihaka au kejeli, ambavyo ndani yake hupelekea watu kucheka au kufurahika na wakati mwengine utani hupelekea watu kukasirika lakini bila ya kuchukuliwa kwa hatua yoyote miongoni mwa watu wanaofanyiana utani huo.

Ngure (2003) katika utafiti wake amefafanuwa *"Migawanyo ya utani katika mafungu matano"* ambayo ni utani kati ya ukoo na ukoo, utani kati ya ndugu na ndugu, utani kati ya makabila na makabila, utani kati ya marafiki na marafiki, na utani kati ya mkoa na mkoa. Mawazo ya mtafiti huyo yamemuongoza vyema mtafiti kubaini kwamba utani upo wa matapo ya namna tafauti. Katika kulidhihirisha hili mtafiti amebaini kwamba kwenye masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba utani upo wa marafiki wa rika moja na wanaofanya shughuli za namna moja.

Ponera (2010) katika utafiti wake unaozungumzia *"Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana yake, sababu za kutumiwa na athari zake kwa wasomaji"*. Anasema kuwa utani ni kipengele muhimu na maarufu sana katika maisha ya jamii nyingi za hapa Tanzania. Umaarufu huo na kuzoeleka kwake kunasababisha

kuonekana kama kipengele cha lazima katika jamii hizo. Kupitia kwa utafiti huo kumemsaidia mtafiti kubaini kwamba kwenye utani unaotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kuna mambo muhimu yanayopatikana katika utani ambayo ndani yake huibua maonyo, mafundisho na burudisho, ambavyo ni moja katika vipengele muhimu katika jamii zetu za Kizanzibari.

Kwa muktadha wa kazi alizopitia mtafit ni dhahiri kwamba katika jamii zetu za Kitanzania upo utani wa aina nyingi, kwa mfano, Utani kati ya kabila na kabila, utani kati ya babu au bibi na wajukuu zake, utani kati ya shemegi mtu na mashemegi zao. Utanihufanyika sehemu mbalimbali za kazi, mfano, mahotelini, maofisini, mashambani, machimboni na masokoni. Katika utafiti huu, mtafiti amedhamiria kujikita zaidi kutafiti dhamira za lugha yautani unaofanyika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Kwasababu mtafiti alibaini kwamba katika sehemu nyingi za masoko ya kuuzia samaki hujitokeza utani kwakiwango kikubwa katika kujenga uhusiano mwema miongoni mwa wanajamii hao.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Mada ya utani imefafanuliwa kwa mawanda mapana katika tafiti nyingi zilizotangulia. Hata hivyo, mada inayohusu *“Kuchunguza dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba”* kwa kiasi anachoelewa mtafiti bado haijafanyika. Kitendo hicho kimempa fursa mtafiti kujikita katika sehemu hizo ili kubaini ni dhamira zipi zinazojitokeza katika lughaya utani inayotumika katika sehemu hizo. Miongoni mwa wataalamu hao ni: Suta na Mnyamba (1999), Ngure (2003), Mc Connel-Giner (2005), Liao (2006), Mgakazi (2010), Mzandi (2011), Kurachie (2012), Gora (2015) na Massoud (2018). Kwa mfano; Suta na Mnyamba

(1999) katika mada inayoitwa “*A Case of reproduction and articulation of utani among the Bena ethic Group in Tanzania*” walichunguza jinsi utani ulivyochangia amani na utangamano miongoni mwa wanajamii wa Bena hapa nchini Tanzania. Katika utafiti huo walieleza jukumu la utani kuwa ni kuimarisha uhusiano mwema miongoni mwa jamii.Kwa hivyo tunaweza kusema kwamba, utani ulitumika katika kutatua migogoro ya Wabena, sambamba na kufunza maadili mema na kuonesha nafasi ya vijana katika jamii. Vile vile walieleza mahusiano ya utani kulingana na mabadiliko ya kiuchumi. Sambamba na hilo utafiti uliofanywa na Rashidi (2011) unaosema: “*Athari za Lugha ya Utani kwa Jamii ya Wapemba, Zanzibar*” unaohusu maeneo ya utani unavyotumika Pemba, alibaini kwamba katika utani kunachukuwa nafasi kubwa kwenye sehemu za kazi. Hivyo basi kupitia kwa kazi hizokulimsaidia mtafiti kupata mwelekeo mpya wa kufanikisha malengo ya kazi yake na kubaini kuwa, kwenye utani kunaimarisha mahusianona kutatua migogoro, kufunza na hata kuimarisha maadili bora katikajamii husika. Hata hivyo, kazi za watafiti hao hazikugusia kuhusu mada: “*Kuchunguza Dhamira za lugha ya Utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba*”. Jambo hilo limempa mwanya mtafiti kuweza kubaini pengo hilo na kuamua kufanya utafiti kuliziba.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yamegawanywa sehemu mbili: Lengo kuunaMalengo mahsusi.

### 1.4.1 Lengo kuu

Kuchunguza dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

i. Kuchambua dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba.

ii. Kubainisha mbinu za kisanaa za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Ili kufikia malengo ya utafiti yaliyowekwa mtafiti wa kazi hii atalazimika kujibu mawili yafuatayo:

i. Ni dhamira gani za lugha za utani unaojitokeza katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba?

ii. Ni mbinu zipi za kisanaa za lugha ya utani zimebainishwa katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unaumuhimu mkubwakwamtafiti mwenyewe, lakini hata kwa watu wengine ambao wataweza kuusomakupitia maeneo mbali mbali kama ifuatavyo:

Kwanza; katika nyanja za kitaaluma, utafiti huu unatarajiwa kuwasaidia watafiti wengi wa baadae watakaojikita kwenye dhana hizi au zinzokaribiana nazo. Watafiti hao wanatarajiwa kuutumia utafiti huu kama chanzo cha kujipatia maarifa katika kazi zao zitakazohusiana na mada kama hii. Walimuwa taaluma ya Fasihi nao kwa upande wao watatumia utafiti huu kama kitabu rejea kufundishia wanafunzi wao katika somo la Fasihi. Wanafunzi wa ngazi mbalimbali kwa kiwango kikubwa watatumia utafiti huu kama nukuu muhimu katika taaluma yao ya kifasihi.

Pili, utafiti huu utakuwa na maslahi makubwa kijamii, kwani inatarajiwa jamii ya Kipemba kupata uelewa mpyana kuweka kumbukumbu juuya utani unaofanywa katika masoko ya kuuzia samaki. Kupitia utani huo jamii itapata uelewa kujuwa kwamba utani ni sehemu muhimu katika maisha ya jamii, hivyo unapaswa kuenziwa, kuthaminiwa na kuheshimiwa kwasababu kila jamii inaishi kulingana na mila maadili na utamaduni wake.

### 1.6.1 Kwa Matumizi ya Nadharia

Kwa upande wa nadharia utafiti huu utasaidia kutanuwa maarifa na kuongeza ujuzi kwa matumizi ya nadharia katika shughuli mbali mbali za kitaaluma na kijamii.Hii inatokana na ufafanuzi wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya Simiotiki jinsi zilivyojadiliwa, kuchambuliwa na kutumiwa katika utafiti huu.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umedhamiria kujikita zaidi katikamada"*Kuchunguza Dhamira za Lugha ya Utani katika Masoko ya Kuuzia Samaki Kaskazini Pemba."*Masoko hayo ni baadhi ya masoko yanayopatikana katika mkoa wa Kaskazini Pemba. Katika wilaya ya Micheweni, masoko matatu yalitumiwa katika utafiti huu. Masoko hayo ni Soko la kuuzia samaki lililoko Shumba ya Mjini, Soko la kuuzia samaki lililoko Tumbe na Soko la kuuzia samaki lilioko Msuka. Katika wilaya ya Wete kuna masoko mawili, ambayo ni Soko la kuuzia samaki lililoko Wete bandarini, na soko la kuuzia samaki lililoko kisiwani Kojani. Hivyo mtafiti katika kazi hii alijishughulisha zaidi katika maeneo hayo kwasababu ndio maeneomahususi aliyolenga na kupata data za kutosha za kuweza kujibu maswali yake na kufanikisha malengo ya utafiti wake. Mtafiti

hatajishughulisha na masoko mengineyo yaliyoko katika mkoa wa Kaskazini Pemba, na hata mkoa wa Kusini Pemba au kwengineko.

## 1.8 Muundo wa Utafiti

Mada ya utafiti huu inahusu: *Kuchunguza dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba* .Ripoti ya utafiti huu imejigawa katika sura tano kama zifuatavyo: Sura ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla wenye vipengele vya msingi vinavyohusu utafiti wowote wa kitaaluma. Vipengele hivyo ni pamoja na usuli wa mada,tatizo la utafiti,malengo ya utafiti,maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa utafiti.

Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Vipengele vilivyogusiwa katika sura hii ni pamoja na ufafanuzi wa istilahi mbalimbali muhimu, mapitio ya kazi tangulizi kuhusu utani, pengo la utafiti na mkabala wa kinadharia.

Sura ya tatu imewasilisha mbinu**za** utafiti**:** vipengele vilivyohusika na eneo hili ni pamoja na maana ya mbinu za utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za uchambuzi wa data na maadili ya utafiti.

Sura ya nne imehusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti: katika sura hii uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti umefanyika kulingana na malengo na maswali ya utafiti huu. Utafiti huu umechambua dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Vilevile sura hii imebainisha mbinu za kisanaa za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kwa kurejelea na nadharia ya Simiotiki.

Sura ya tano ilihusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo: Sura hii imetowa muhutasari wa utafiti huu, hitimisho na mapendekezo kwa tafiti za baadaye. Miongoni mwa mapendekezo hayo endapo yatazingatiwa, yanaweza kusaidia vyema kuibuwa hisia mbali mbali zenye umuhimu katika utafiti huu na tafiti nyengine.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika utafiti huu, mtafiti amewasilisha ufafanuzi wa istilahi mbalimbali zenye muhimu katika sura hii. Pia mtafiti ametalii na kuwasilisha vipengele mbalimbali vilivyohusu kazi tangulizi kulingana na mahitaji ya utafiti wake. Pengo la Utafiti na mkabala wa kinadharia ni miongoni mwa vipengele vilivyowasilishwa na kufafanuliwa.

## 2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu

Katika sura hii, mtafiti amefafanua istilahi mbali mbali, muhimu ambazo zimetoa mwanga katika utafiti wake. Miongoni mwa istilahi hizo ni pamoja na: Maana ya utani, dhamira pamoja na mbinu za kisanaa. Ufafanuzi huu ulikuwa na malengo ya kumfanya msomaji wa utafiti kuelewa kwa urahisi malengo ya utafiti huu ili kuweza kupata kwaurahisi kwa ambalo alihitaji kupata msaada utakaohitajika kuhusiana na kazi yake.

### 2.2.1 Maana ya Utani

Wamitila (2003) anaelezakuwa utani ni dhana inayotumiwa kueleza hali ya kufanyiana mzaha miongoni mwa wanajamii au jamii mbali mbali bila kuogopa au kushitakiana. Ngure (2005) anasema kwamba utani ni fani ya kipekee katika fasihi simulizi na inasehemu kubwa katika maisha ya kila siku. Aghalabu utani hufanywa kwa njia ya malumbano ambapo mtu mmoja huanza kwa kumtania mwengine na kujibiwa hapo hapo. Aidha, anasisitiza kuwa watu wanaweza kutaniana harusini, ngomani, katika hadhara ya pombe na hata matangani. Rashid (2011), ameeleza

kuwa utani nimaneno na kutendeana vitendo vinavyokubalika kwa jamii hiyo, iwe dhihaka au masihara. Katika utani kunakuwa hakuna chuki inayoweza kuibuka kutokana na maneno hayo. Ngure (2003), ameifafanua migawanyo ya utani katika mafungu matano: utani kati ya koo na koo, utani kati ya ndugu na ndugu, utani kati ya kabila na kabila, utani kati ya rafiki na marafiki zao, na utani kati ya watu wa mkoa na mkoa.

Mtafiti amedhamiria kuzungumzia utani kati ya rafiki na marafiki zao walioko katika maeneo ya masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Mtafiti ameamua kutafiti eneo hili kwa sababu kwa kiasi anachoelewaameona ni sehemu ambayo haijafanyiwa kazi vizuri na ni sehemu muhimu katika maendeleo ya jamii. Kwa ujumla mtafiti anaona kuwa utani ni vitendo vya watu kufanyiana mzaha, masihara, vijembe au kejeli, ambavyo ndani yake hupelekea kuibuka furaha, na wakati mwengine huibuwa hasira pasi na kuchukuliwa hatua yoyote.

### 2.2.2 Maana ya Dhamira

Wataalamu mbalimbali wamejitahidi kufafanua maana ya dhamira.Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na hawa wafuatao; Wamitila (2002), anasema dhamira katika kazi ya fasihini mawazo makuu ambayo msanii amekusudia kuyawasilisha kwa jamii ili iweze kuadilika. Senkoro (2011) anasema kuwa katika dhamira kuu, tunaweza kugundua dhamira ndogo ndogo zinazoambatana na dhamira kuu. Kwa kawaida dhamira hulenga katika nyanja mbalimbali za maisha ya mwanadamu kama vile nyanja za kiuchumi, utamaduni, kisiasa, kijamii na nyenginezo ambapo kimsingi hutegemeana na mguso au hisia za msanii ambazo hutegemeana na wakati. Kwa ujumla mtafiti ameona kwamba dhamira ni fikra kuu, mawazo makuu, ambayo

humpelekea msanii kufikia lengo husika ambalo limejitokeza katika kazi za kifasihi. Mtafiti alidhamiria kuonesha dhamira zinazojitokeza katika lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ikiwa ndiyo lengo kuu la utafiti wake.

### 2.2.3 Maana ya Mbinu za Kisanaa

Senkoro (2011) anasema kuwa matumizi ya lugha ni moja wapo miongoni mwa matumizi ya mbinu za kisanaa zinazotumiwa na watunzi mbali mbali kwa kazi za fasihi. Abourweeshah (2017) anaeleza kuwa mbinu za kisanaa ni ufundi wa kisanaa unaotumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi katika kuijenga kazi yake. Ufundi huo hutegemea mbinu za kisanaa ambazo mtunzi anazitumia katika kazi yake na mara nyingi humtofautisha na waandishi wengine. Mbinu hizo za kisanaa hupatikana ndani ya vipengele vya fani katika kazi ya fasihi ikiwa ni pamoja na matumizi ya lugha, wahusika, mandhari, mtindo na muundo.

Kwa ujumla, mtafiti ameona kuwa mbinu za kisanaa ni stadi ya hali ya juu iliyomo ndani ya kazi za kifasihi zinazotumiwa na mwandishi katika kazi yake kwa lengo la kuipamba kazi hiyo ili ilete mvuto kwa jamii husika pamoja na kufikisha ujumbe uliokusudiwa inavyostahiki. Hivyo basi kwa mnasaba wa mada ya utafiti huu kupitia lengo mahsusi la pili, mbinu za kisanaa ambazo zimekusudiwa kuwasilishwa, kubainishwa na kuchambuliwa zimehusu: Matumizi ya lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Mbinu hizo ni pamoja na matumizi ya tashbiha, taswira, takriri, ishara, kejeli, misemo, majazi, methali na tashtiti.

## 2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizikuhusu Utani

Dhana ya utani imezoeleka sana katika jamii za watuduniani. Wapo watu ambao ni maarufu na walikuwa wakitumia utani kwa karne nyingi zilizopita. Tafiti nyingi

zilizofanyika zimejitahidi kuelezea utani kwa mitazamo tofauti jinsi unavyoweza kutumika. Miongoni mwa kazi tangulizi zilizohusu utani katika maandiko yaliyopita ni kama zifuatazo:

Mehrabin na Pierce (1993), katika utafiti wao wenye mada "*Differences in Positive and Negative Connotations of Nicknames and Given Names"*waliangalia majina ya utani na majina halisi ya watu. Utafiti huu ulihusu jamii ya wasomi katika nchi ya Iran. Watafiti hao waligundua kuwa kila aina ya majina yana umuhimu katika nafasi yake. Kwa mfano, majina halisi ya watu yana hadhi kubwa zaidi na mafanikio na kujenga hamasa na fikra nzuri zaidi katika sehemu za kazi na ujuzi wa kitaalamu, lakini majina ya utani hadhi yake inalenga zaidi juu ya kujenga umaarufu na kufurahisha. Kazi ya Mehrabian na Pierce (wameshatajwa) imemsaidia sana mtafiti katika mada yake inayolenga kuchunguza dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Msaada alioupata kwenye utafiti huu ni kutambua athari na dhima za majina ya utani katika jamii ya watu wa Iran na kwa hivyo atapata kuchunguza pia athari za majina ya utani katika jamii ya Wapemba, jambo lililompa mtafiti mwelekeo mkubwa wa kufanikisha kazi yake.

Shankle (1995) ametafiti mada: "*American Nick names*; *Their Origin and Significane*." Utafiti wake Shankle (keshatajwa) aligunduwa kuwa jamii ya Wamarekani wengi ni watu wanaopenda utani zaidi kuliko jamii nyengine nyingi. Aidha, Wamarekani hao wanakawaida ya kuwapa majina ya utani wake zao, waume wao, watoto wao, marafiki wao, lakini hata maadui zao na hivyo ni mwiko kwao kuwepo na mtu mtakatifu ambaye anaweza kuwa hana jina la utani. Utafiti huu umemsaidia mtafiti kutambua kuwa kumbe si jamii ya wanaume tu wenye kawaida

ya kutumia utani, lakini hata jamii ya wanawake wanahusika kwa kiasi kikubwa katika kutumia dhana hii ya utani. Aidha, mtafiti ameweza kugunduana kupata mwanga mkubwa juu ya dhana hii ya utani kwa jamii ya Wamarekani. Amegundua pia majina ya utani ya Wamarekani ni ufupisho unaotoka na majina yao halisi. Kwa hivyo kazi hii imekuwa ni dira muhimu sana kumuwezesha mtafiti kufikia malengo ya utafiti wake wa mada husika, ambayo inahusika na Kuchunguza dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba.

Kiesling (1997) alifanya utafiti katika mada *"Power and the Languageof Men*" Utafiti huo uliangalia majina ya utani katika taasisi za elimu huko Marekani. Aligundua kuwa mazungumzo ya utani yalitumikasana kwa wanaume kuliko wanawake. Utafiti huo wa Kiesling (ameshatajwa) haukuzingatia utani unaotumika katika masoko ya kuuzia samaki. Kupitia na kuudurusu utafiti huo kulimsaidia mtafiti kuelewa utani ambao hutumika zaidi katika jamii ya wanaume kuliko jamii ya wanawake. Jambo hili limemsaidia mtafiti katika utafiti wake kubaini kwamba watumiaji wakubwa wa lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ni wanaume kuliko wanawake.

Waziri na Dlourine (1998) katika mada yao isemayo "*The Case of Reproductin and Articulation of Utani among the Pare in Tanzania",* waliangalia jinsi utani ulivyochangia amani na utengamano katika jamii ya Wapare iliyoko Kaskazini mwa Tanzania. Katika utafiti wao walieleza asili ya utani katika jamii ya Wapare kuwa ni vita vya kikabila. Walitoa mifano kuhusu baadhi ya asili za neno yanayotumika katika jamii zao. Neno "*Pare*" kwa mujibu wa maelezo waliyoyatoa limetolewa na Wachaga wakiamanisha *"Mpige".* Hali hii ilisababisha wakaazi wa nyanda za juu

Kaskazini mwa Tanzania kuitwa Wapare. Huu ndio mwanzo wa uhusiano wa kutaniana baina ya makabila haya mawili. Katika maelezo hayo ya Waziri na Dlourine (wameshatajwa) itagundulikana kuwa jina la "Pare" limeibuka zamani kutokana na utani. Kazi hii imemsaidia mtafiti kubaini kwamba katika makundi mbalimbali ya jamii ya watu wanaofanya shughuli za namna moja kunakuwa na matendo au lugha za utani zinazotumika miongoni mwao. Kwa hivyo katika masoko ya kuuzia samaki hali hii ya matumizi ya lugha ya utani hujitokeza kwa kiwango kikubwa. Jambo hili limemsukuma mtafiti wa kazi hii kushughulikia eneo hilo.

Mc.Connel-Giner (2005) katika utafiti wake wenye mada *"What's in a names Social labeling"* anaeleza kuwa wanaume ndio wenye majina ya utani zaidi kuliko wanawake. Dhana hii pia imeungwa mkono zaidi na Liao (2006), kwenye utafiti wake wenye mada isemayo *"Linguistic Analysis of Nicknames of Junior High School Students Taiwan"*. Katika utafiti wake aligundua kuwa katika shule aliyoifanyia utafiti ya Feng Dong ya Taiwan yenye wanawake 152, kati yao 119 sawa na asilimia 78.29 wana majina ya utani. Pia kati ya wanaume 142, kati yao 131 sawa na asilimia 91.61 wana majina ya utani. Vile vile aligundua kuwa kati ya madarasa manane (8) ya shule hiyo, takribani madarasa matatu (3) yanaweza kuwa na wanafunzi wenye majina ya utani wakiwamo wanawake na wanaume. Utafiti huo umemsaidia mtafiti kubaini kwamba katika sehemu yoyote ya mikusanyiko ya watu kunakuwepo na utani miongoni mwao. Hivyo basi ni dhahiri katika utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba*, alitabiri kwambakungeweza kumsaidia kupata utani wa aina nyingi kwasababu kuna mikusanyiko mingi ya watu wanaofanya kazi katika masoko ya

kuuzia samaki. Watu hao bila shakaniwatumiaji wazuri wa lugha ya utani katika shughuli na mazingira yao ya kikazi.

Mgakanzi (2010) anaufafanua utani wa jamii ya Kisukuma jinsi unavyotendeka kwa kusema kuwa utani hufanywa kupitia usimulizi, nyimbo, matendo, furaha na hadithi ndefu. Vilevile Mgakanzi (keshatajwa), ameonesha baadhi ya maeneo ambayo hufanyika utani huo. Ameyataja maeneo hayo kwamba ni pamoja na sehemu za sherehe za harusi. Katika sherehe hizo watani hufanya utani wao na kuendelea nao mpaka pale wanapopewa pesa. Pindi wanaponyimwa pesa hufanya fujo katika sherehe hiyo. Kazi hiyoimemsaidia mtafiti kujua kwamba utani unaotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba huchukuwa nafasi kubwa katika njanja nyanja tofauti, kama vile matendo, majina na misemo.

Mzandi (2011) katika utafiti wake ametafiti "*Mahusiano ya kibiashara katika utani, kati ya Wahehe na Wangoni*". Utafiti huo ulilengakutazama namna matendo ya kiucheshi yanavyofanyika wakati wa kuuza na kununua. Jambo hili mtafiti limempa msaadamkubwa wa kubaini kwamba shughuli nyingi za kijamii zinazotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba zinatawaliwa na utani kwa kiasi kikubwa, hii ni kutokana na kwamba moja kati ya dhamira kuu ya utani ni kuibuwa ucheshi miongoni mwa jamii husika. Kwa hivyo utafiti wa Mzandi (ameshatajwa) umezidi kutilia mkazo na kuimarisha mada ya utafiti huu kwa mnasaba wa malengo na maswali ya utafiti huu.

Zaid (2011) ametafiti *"Athari ya lugha ya utani kwa jamii ya Wapemba"* Katika utafiti wake ameeleza kuwa katika kisiwa cha Pemba utani bado una nafasi kubwa na muhimu katika maisha ya kila siku. Akaendelea kusema kuwa utani umechukuwa na

kutawala sehemu kubwa katika nyanja zote za maisha. Aidha anafafanua zaidi kwa kusema kuwa utani umetawaliwa na semi mbali mbali zenye kuashiria kejeli, dhihaka, matusi na hata dharau. Utafiti huu umemsaidia kugundua kwamba kwenye utani hutumika lugha maalumu ambazo hupelekea kuchochea utani huo. Kutokana na dhana hiyo ni dhahiri kwamba hata kwenye masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba lugha za matusi, kejeli, dhihaka na dharau hujitokeza na hutamba kwa kiasi kikubwa kwa mnasaba wa kuchochea uvumilivu na mashirikiano sehemu ya kazi.

Kuranchie (2012) alifanya utafiti katika mada *"Student's Nick Names .Their Source and Effects on Learning".* Utafiti huo uliangalia majina ya utani naathari za majina hayo kwa wanafunzi katika kujifunza. Sambamba na hilo utafiti huo uligundua kuwa majina ya utani yanatumika katika shule nyingi nchini Ghana kama ambavyo hutumika katika nchi nyengine. Vile vile katika utafiti wake Kuranchie (ameshatajwa) aligunduwa kuwa takribani asilimia 77.02 ya majina ya utani yanatumiwa na wanafunzi wa elimu ya juu, hasa hasa kwa wanaume ingawaje utumiaji huo wa majina ya utani unaathiri muelekeo wao wa kujifunza hasa wakati wa kujibu maswali darasani,kutoa maoni yao na kujieleza.Kazihii ilitoa mwanga mkubwa kwa mtafiti katika kufanikisha malengo ya utafiti wake, na kubaini kwamba kwenye utani hupelekea athari ambazo ndani yake kwa watu wanaosoma hukosa fursa kadha za kujifunza kati yao. Kwa hivyo katika utafiti huu sehemu za masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kunajitokeza lugha mbali mbali za utani ambapo ndani yake hupelekea kuwepo kwa athari miongoni mwaokwasababu asilimia kubwa ya watu wanaofanya kazi sehemu hiyo hutumia lugha au matendo mengi ya utani kwa lengo la kujenga uhusiano mwema kati yao.

Gora (2015), katika utafiti wake kuhusu mada ya *“Utani katika sherehe za harusi za Watumbatu”* alifafanua na kuibuka na changamoto kadhaa zinazopelekea kupotea kwa amali ya utani kwa jamii ya Watumbatu. Hali hiyo ilimsukuma mtafiti kuchunguza aina, sababu na taashira za utani katika sherehe za harusi za Watumbatu kwa lengo la kuendeleza na kuenzi utani kama ni amali muhimu ya kijamii.Utafiti huo umemsadia mtafiti wa kazi hii kubaini kwamba suala la utani ni moja kati ya amali muhimu ya utamaduni wa Kizanzibari, hivyo utani unaofanyika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ni vyema kutunzwa, kuthaminiwa, kuuenziwa na kuendelezwa kwa manufaa ya kizazi cha baadae na Taifa kwa ujumla.

Massoud (2018) katika utafiti wake unaohusu *“Tathimini ya maana na vigezo vilivyotumika kutoa maana ya utani kwa jamii ya Wapemba,”* hakutaja utani unaotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba lakini ametoa mwanga mkubwa kwa mtafiti na kubaini kwamba katika utani kunakuweko na vigezo maalumu vinavyotumika katika jamii husika. Hivyo, mtafiti amebaini kwamba miongoni mwa vigezo vya utani vinavyotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ni pamoja na rika, jinsia, umri na watu maalumu. Kwa kawaida watumiaji hasa wa utani katika sehemu za masoko ya kuuzia samaki huwa ni madalali, wavuvi, wanunuzi na hata wajasiriamali wadogo wadogo. Na pindi ikitokezea utumikaji wa utani huo kwa mtu mgeni haichukuliwi kama ni kosa, bali huhesabiwa kuwa ni miongoni tu mwa utamaduni, mila na desturi za sehemu hizo. Utafiti huo uliweza kuainisha vigezo vinavyojitokeza kutoa majina ya utani katika Kiswahili kwa jamiiya Wapemba. Kazi hiyo iliweza kumsaidia mtafiti kubaini kwamba katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba, utani unaotumika

unahitaji vigezo maalumu katika utumiaji wake na humsaidia mtafiti kufanya kazi yake kwa ufanisi zaidi katika kukamilisha malengo ya utafiti wake, sambamba na kupata jawabu ya maswala ya utafiti huo. Kwa hivyo kwa mujibu wa kazi tangulizi za watafiti huu ni wazi kuwa kazi hizo zimeweza kumsaidia sana mtafiti kuweza kutambua dhana hii ya utani kadri inavyoweza kutumika kwa jinsia zote mbili kati ya kike na kiume. Aidha, kazi hizo zimekuwa kama dira iliyoongoza kwenye mafanikio katika kufikia kwenye malengo mahususi na kuweza kujibu maswali ya utafiti huu. Pamoja na jitihada kubwa zilizofanywa na watafiti waliotangulia, mtafiti hakubaini kabisa utafitiuliofanywa kuhusu utani unavyojitokeza katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Kwa muktadha huo mtafiti wa kazi hii ameamua *Kuchunguza dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba* ili kuziba mwanya ulioachwa na watafiti tangulizi.

## 2.4 Pengo la Utafiti

Katika kupitia na kuchunguza kazi tangulizi zinazohusiana na utani, mtafiti amebaini kazi mbalimbali zilizofanywa zinahusiana na mada ya utafiti huu. Miongoni mwa kazi hizo ni ile ya Ngure (2003), Mc- Connel- Giner (2005), Rashid (2011), Mgakazi (2010), Mzandi (2011) na Zaid (2011). Kazi hizi zilikuwa na manufaa pamoja na mchango mkubwa mno katika kuendeleza utafiti wa kazi hii. Pamoja na mchango, mtafiti amebaini kwamba bado hakuna utafiti wowote ambao umefanyika kuhusu mada: *Kuchunguza dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba.* Kwa hivyo kuwepo kwa pengo hilo kumemsukuma mtafiti kufanya utafiti huu kwa kuzingatia malengo na maswali ya mada ya utafiti huu inavyostahiki ili kuziba pengo la utafiti lililoachwa na watangulizi wake.

## 2.5 Mkabala wa Kinadharia

Katika uandishi wa kazi ya utafiti, ni dhahiri kwamba kuwepo kwa matumizi ya nadharia stahiki ni jambo lisilopingikanadharia ulimwenguni zipo nyingi na kila nadharia inaubora wake na wakati mwengine huwepo na baadhi ya mapungufu. Kwa mantiki hiyo uteuzi wa nadharia stahiki utasaidia sana katika uchambuzi mzuri wa mada ya mtafiti. Kwa muktadha huo mtafiti ameteuwa na kutumia Nadhania mbili ambazo ni nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayolenga kwenye lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu. Nadharia ya pili iliyoteuliwa ni Simiotiki ambayo imekusudiwa kutumika kwenye lengo mahsusi la pili na swali la pili la utafiti kwa kuamini kwamba nadharia hizo zinafaa katika uchambuzi wa data za utafiti.

## 2.6 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Wataalamu mbali mbali wamezungumzia kwa kina juu ya ya nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Miongoni mwa wataalamu hao ni Wamitila (2002), ambaye anaeleza kuwa Mwitiko wa Msomaji ni nadharia inayorejelea mitazamo au tabia fulani za msomaji wa matini unaohusisha uhakiki wa aina mbali mbali ambayo huanza kwa dhima na majukumu ya msomaji katika matini au katika kazi za kifasihi. Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kuwa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji husisitiza nguvu za msomaji na nadharia hii iliasisiwa na wahakiki na wataalamu wa Kijerumani mwishoni mwa miaka ya 1960 na mwanzoni mwa miaka 1970. Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Robert C. Holub, Hans Robert Jauss na Wolfagang Isser.

Haji (2017) katika utafiti wake uliohusu *"Kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mfano kutoka Makunduchi"* anasema kwamba, lengo

kuu la nadharia hii ya Mwitiko wa Msomaji ni kuwachunguza na kuwabainishia wasomaji pamoja na usomaji wake. Wahakiki wengi wanaojishughulisha na nadharia hii mara nyingi huwa na mtazamo tafauti na ule wa kijadi unaoangalia fasihi kwamba ni kitu kilichokamilika. Kwa hivyo maana yoyote ya kifasihi hutegemea msomaji wake. Vile vile msomaji anaweza kusawiriwa na kuonekana ana mchango mkubwa wa kubuni maana ya kazi ya fasihi. Hii ina maana ya kwamba si kitu kirahisi kudai kuwa kuna maana fulani ndiyo sawasawa sawa na sahihi zaidi. Wasomaji wengi wanaweza kuvifasiri vipengele vya kiisimu na kisanaa kwa mbinu mbalimbali kupata maana tofautitofauti katoka katika matini moja. Jambo la msingi ni kwamba hatunabudi kukubaliana na fikra na mawazo ya nadharia hii kwa sababu yanampa msomaji uhuru wa kuweza kuisoma kazi, kuielewa na kuihakiki kazi ya fasihi kwa jinsi anavyoweza kulingana na uzoefu na tajiriba yake.

### 2.6.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Wamitila (2002) amefafanua mihimili ya nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kama ifuatavyo:

i) Maana ya kazi yoyote ya kifasihi inamtegemea kwa kiasi kikubwa msomaji wa kazi hiyo. Hii ina maana kuwa ni vigumu kudai au hata kusema kuwa kuna maana fulani ndiyo sahihi kuliko maana maana nyingine ya matini hiyo hiyo moja.

ii) Kuna vipengele vya kimsingi mbalimbali vinavyouunda mwitiko wa msomaji.

iii) Matini husika inaweza kuwa tofauti kwa namna inavyoelekeza au kutatiza mwitiko wa msomaji. Sifa ambayo inazua usomaji mzuri au usomaji mbaya kwa kazi inayohusika.

iv) Ipo tofauti kati ya uasili wa matini husika na hisia za kibinafsi za msomaji anayehusika.

Nadharia hii ilijipatia mashiko na sifa kubwa zaidi mwishoni mwa miaka ya sitini na sabiini baada ya kuwekewa misingi yake na wanazuoni wakuu kutoka Chuo Kikuu cha Constance huko Ujerumani. Uchunguzi mpya ulisisitizwa kuhusu usomaji na upokezi wa matini za kifasihi.

### 2.6.2 Sababu ya Uteuzi wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Mtafiti ameona kuwa nadharia hii ni muwafaka zaidi na inaweza kufikisha lengo lake la kwanza la utafiti wake. Mtafiti alitumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika kuchambua data za lengo mahususi la kwanza la utafiti pamoja na suala la kwanza la utafiti ambalo kwa ujumla wake linahusu: Kuchambua dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Lengo la pili na swali la pili la utafiti lilichambuliwa kwa kutumia nadharia ya Simiotiki.

### 2.6.3 Nadharia ya Simiotiki

Ferdinand de Saussue na Charles Pierce (1966) ni waasisi wa nadharia hii ya Simiotiki. Katika nadharia hii Saussue anaeleza dhima ya ishara katika jamii, wakati Pierce anazungumzia maana na hali halisi ya lugha ya ishara jinsi inavyohusiana kimantiki na utamaduni wa jamii fulani kwa mnasaba wa kutowa maana maalumu. Wamitila (2002) akiwanuu Blamires (1991), Geoffrey na wenzake (1988) wakisema kwamba matini moja yaweza kuwa na fasili nyingi zinazolingana au kukinzana na zote zikakubalika.

Wamitila (2002) anasema nadharia hii inatumika sanakatika uchambuzi wa kazi za fasihi, ambapo kimsingi hushughulikia ishara na uashiriaji. Ishara nyingi zinazojitokeza katika kazi za kifasihi huundwa na mtunzi mwenyewe (msanii) kwa kuzingatia muktadha wa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Vile vile anaendelea kusema kuwa katika lugha kuna vitu viwili, navyo ni *kitaja* yaani umbo ambalo alama inachukuwa na *kirejelee (a signified)* yaani maana inayowakilishwa na alama hiyo. Kwa mantiki hiyo tunapata uelewa kuwa, kuna kitaja na kirejelea, ambapo mahusiano kati yao ni ya kubuni tu, na hutegemea utamaduni wa jamii husika. Licha ya kuwa inawezekana kuwa na uhusiano kati ya kitaja na kirejelea. Lakini kama wanajamii wamekubaliana juu ya matumizi yake basi hutumika na kuelewana miongoni mwao.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa mfumo huu ni sehemu ya utamaduni japo imekabidhiwa mipaka maalumu na maumbile kama lugha. Nadharia hii imejengwa kwa mihimili mitano, ikiwa ndiyo misingi mikuu katika kuzifumbua ishara zilizotumika katika kazi ya fasihi. Misingi hiyo ni muktadha, ujumbe, msemaji, mpokeaji na lugha.

**2.6.3.1 Misimbo ya Nadharia ya Simiotiki**

Wamitila (2002) akimnukuu Barthes (1994) akieleza kuwakuna aina tano za misimbo zinazotumika katika kazi za kifasihi. Aina tano hizo za misimbo ndizo ambazo kwa pamoja huunda Nadharia ya Simiotiki. Mhakiki huyu alizuka na dhana hii kupendekeza jinsi bora ya kuisoma kazi ya kifasihi au matini ya kifasihi.Lengo la Barthes (ameshatajwa)ni kuivunja matini ya kifasihi kwenye sehemu ndogo ndogo alizoziita Leksia.Hivi ni kama vitengo vidogo vya kisomaji ambavyo vinaurefu sawa,

ambapo kila leksia hudhihirisha misimbo au kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri.Aina tano kuu za misimbo imeishia kuitwa “Misimbo ya usomaji” na ni nguzo muhimu katika nadharia hii.Aina hizo za misimbo ni msimbo wa kimatukio, kihementiki, kiseme, kiishara na kirejelezi.

**Mosi; Msimbo waKimatukio:** Msimbo huu unahusu jinsi ya matukio yanavyoungana na kushonana, kusababishana au kuathiriana katika kazi husika. Imezoeleka kuwaona wataalamu wengi wa Fasihi ya Kiswahili wakihusisha kazi zao nadhana hii ya matukio ambayo hujitokeza.

**Pili; Msimbo wa Kiishara:** Huu ni msimbo anauutumia msomaji katika kuhakiki kazi za kifasihi na unahusishwa kwa namna anavyochambua maana za kiishara katika kazi za kifasihi. Vilevile msimbo huu unahusishwa na msomaji na mhakiki kwa namna wanavyohakiki na kuchambua matendo na kazi za fasihi zote zinazotumia ishara.

**Tatu; Msimbo wa Kiseme:** Neno *kiseme* asili yake linatokana na neon *“sema”* linalotumiwa kuelezea elementi nasibishi ya kisemantiki, ambapo elementi hizi zina tuwezesha kupata picha fulani, kutokana na viashiria fulani ambavyo hupelekea kuelewa sifa kamili ya tukio, jambo, hali au mhusika fulani wa kazi ya kifasihi.

**Nne; Msimbo wa Kihemenitiki:** Msimbo huu unahusu taharuki na unajulikana na baadhi ya wahakiki kama msimbo wa kusimulia hadithi / usimulizi. Vilevile msimbo huu unaweza kufumbatwa kwenye anwani ya kazi za kifasihi. Anwani hiyo inaweza kuwa jina la kitabu, shairi na igizo.

**Tano; Msimbo wa Kirejelezi:** Msimbo huu unajengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelewa katika kazi inayohusika ya kifasihi. Urejelezi huu huunda uhalisi mahususi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka kwa msomaji na kwa njia hiyo huipa kazi fulani nguzo za kiutamaduni.

#### 2.6.3.2 Sababu za Uteuzi wa Nadharia ya Simiotiki

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba na hivyo nadharia ya Simiotiki imeteuliwa kutumika katika uchambuzi wa vipengele vya mbinu za kisanaa ikiwa ni lengo mahususi la pili la tasnifu hii. Nadharia hii imetuliwa kwa sababu inahusika na lugha ya ishara, picha, misimbo, taswira na mafumbo kutaja kwa uchache.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura ya pili kumewasilishwa mambo mbalimbali yanayohusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Mambo yaliyowasilishwa ni pamoja na: Ufafanuzi wa Istilahi mbali mbali kama vile maana ya utani na maana ya dhamira. Vile vile mtafiti ameangalia mapitio ya kazi tangulizi kuhusu utani. Pengo la utafiti pia limebainishwa na kuwekwa wazi katika sura hii. Mwishoni mtafiti amechambua mkabala wa kinadharia ambapo nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na Simiotiki zimechambuliwa na kufafanuliwa vizuri.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ilijikita zaidi kufafanua mbinu mbali mbaliza utafiti. Kothari (2003) anafafanua kuwa mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu au taratibu zote stahiki zinazotumika wakati wa kufanya utafiti. Vipengele muhimu vilivyochambuliwa katika sura hii ni pamoja na Maana ya mbinu za utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, mbinu za kukusanya data, mbinu za uchambuzi wa data, maadili ya utafiti na hitimisho.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni sehemu au mahala ambapo utafiti hufanyika kulingana na mtafiti alivyolenga kupata data zake (Cresswell, 2009). Kijiografia eneo la utafiti ni pahala ambapo mtafiti amekusudia kukusanya data za utafiti. Utafiti huu ni wa uwandani na umefanyikakatika kisiwa cha Pemba, mkoa wa Kaskazini, katika masoko ya kuuzia samaki yaliyoko Tumbe, Shumba Mjini na Msuka katika wilaya ya Micheweni na soko la kuuzia samaki Kojani na Wete bandarini lililoko mjini Wete katika wilaya ya Wete. Katika sehemu hizo mtafiti alikusanya data za msingi (awali) zinazohusu dhamira za lugha ya utani katika utafiti wakekwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti. Maelezo kuhusu idadi ya watafitiwa katika masoko yaliyohusishwa katika utafiti huu yamefafanunuliwa vyema na jadweli lifuatalo:

**Jadweli 01: Muhutasari waIdadi ya Watafitiwa katika Masoko ya kuuzia Samaki Kaskazini Pemba**

| **Na** | Soko | Wanawake | Wanaume | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| **1** | Kojani | 04 | 06 | 10 |
| **2** | Msuka | 04 | 06 | 10 |
| **3** | Shumba Mjini | 03 | 07 | 10 |
| **4** | Tumbe | 05 | 15 | 20 |
| **5** | Wete | 05 | 15 | 20 |
| **6** | Jumla | 21 | 49 | 70 |

**(Chanzo: Mtafiti, 2022)**

Data ya jadweli na (01) inaonyesha muhtasari wa idadi ya watafitiwa katika utafiti huu. Idadi ya wanaume ilikuwa ni arobaini na tisa (49) na wanawake walikuwa ni ishirini na mmoja (21). Hii ni kutokana na kuwa idadi ya wanawake katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya wanaume. Kadhalika katika kupata data za upili mtafiti alitumia maktaba kuu Zanzibar, tawi la Chake Chake Pemba, maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, tawi la Pemba, Maktaba ya (SUZA) tawi la Pemba na kwenye wavuti. Mtafiti ameyatumia maeneo hayo ili kupata kumbukumbu za data muhimu ambazo zinalingana na mada yake. Vyanzo hivi vya data za upili viliweza kukidhi mahitaji ya malengo na maswali ya utafiti huu.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Orodho (2003) anasema umbo la utafiti au usanifu wa utafiti ni mpangilio na taratibu zinazotumika kukusanya data na kuchambua data kwa namna ambayo data

zitapatikana na malengo ya utafiti. Kothari (2004) anafafanua Usanifu wa Utafiti ni mpangilio maalumu unaoonesha namna na jinsi utafiti utakavyofanyika ili kuwezesha malengo ya utafiti kufikiwa na kujibu maswali ya utafiti husika ipasavyo. Kombo na Tromp (2006) wanasema kwamba, dhana hii ya umbo la utafiti au usanifu wa utafiti inaweza kutafsiriwa kuwa ni mchoro au ramani inayoonesha namna utafiti utakavyofanyika kuanzia kukusanya data, kuchambua data na kuandika ripoti ya utafiti. Hivyo utafiti huu ulilenga kwenye uchunguzi wa dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Pia mtafiti ametumia mkabala wa kimaelezo kuchambua data kulingana na malengo mahsusi ya utafiti huu.

## 3.4 Kundi Lengwa

Kombo na Tromp (2006) wanasema kwamba, walengwa ni kundi wakilishi la watafitiwa, linaloweza kutowa majibu ya maswala ya mtafiti. Newman (2006) anasema walengwa ni kundi ambalo mtafiti huliteuwa akiwa na mategemeo ya kwamba litampatia data zitakazowezesha kukamilisha madhumuni ya utafiti wake. Katika utafiti huu kundi lengwa ni wanajamii wa Pemba wanaoishi sehemu mbali mbali katika kisiwa cha Pemba hususani mkoa wa Kaskazini Pemba. Watu wanaolengwa hasa ni wale ambao hufanya shughuli zao za kikazi katika masoko ya kuuzia samaki wilaya ya Wete na wilaya ya Micheweni. Sababu kubwa ya mtafiti kuteua kundi lengwa hilo ni kwamba aliamini kuwaatapata taarifa za kutosha kutoka kwa watafitiwa haoambao anaishi nao kwa ukaribu na katika mkoa mmoja. Kwa msingi huo ndio maana mtafiti akaweza kuwafikia watafitiwa mara nyingi zaidi kwa lengo la kwenda kukusanya taarifa anazozihitaji kulingana na mada yake. Ilikuwa ni wepesi kuwapata walengwa wake.

### 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Kothari (2008) anaeleza kuwa sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa na mtafiti kuwakilisha sifa na tabia za kundi zima lililolengwa kutafitiwa. Sampuli humsaidia mtafiti kupata taarifa ambayo humpa majumuisho ya utafiti wake. Kwa upande wa Bryman (2004) anasema kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha watu au vitu, ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi linalotakiwa kufanyiwa utafiti. Sampuli huchaguliwa kwasababu si rahisi kutafiti kundi zima lililokusudiwa kutafitiwa. Kwa ujumla sampuli ni kitu au vitu kati ya vitu vingi vya aina moja vinavyoteuliwa kama mfano au kigezo cha kuwakilisha vitu vingi. Sambamba na hilo, usampulishajini mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu kutoka kwenye kundi lengwa ili litumike kwenye utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa.

Kwa kuwa haikuwa rahisi kwa mtafiti kuwafikia watu wote wanaotumia lugha za utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba, aliteuwa watu kumi (10) katika soko la Kojani, wanaume sita (6) na wanawake wanne (4). Soko la Msuka mtafiti ameteuwa watu kumi (10), wanaume sita (6) na wanawake wanne (4). Soko la Shumba ya Mjini ameteuwa watu kumi (10) wanaume saba (7) na wanawake watatu (3). Katika soko la Tumbe mtafitialiteuwa watu ishirini (20) wanaume kumi na watano (15) na wanawake watano (5). Katika soko la Wete ameteuwa watu ishirini (20) wanaume kumi na watano (15) na wanawak watanoe (5). Kwa hakika uteuzi huu umefanywa na mtafiti kwa mnasaba wa uelewa wa watafitiwa kuhusiana na lugha ya utani na kuwakilisha wengine kwa kila soko, sambamba na kuzingatia malengo na maswali ya mada ya utafiti.

## 3.6 Ukusanyaji wa Data

Omary (2011) anaeleza kwamba mbinu za ukusanyaji wa data ni zile zinazotumiwa na mtafiti katika kupata data za utafiti wake.Anaendelea kufafanua kwakusema kwamba zipo mbinu tofauti ambazo zinaweza kutumiwa katika kukusanya data. Mbinu hizo ni pamoja na uchunguzi makini, hojaji, usaili, mahojiano ya vikundi majaribio na mengineyo. Kwa ujumla ukusanyaji wa data ni mbinu za kupata taarifa ambazo zilimsaidia mtafiti kupata ukweli katika utafiti wake. Hivyo basi katika utafiti huu, mtafiti alikusanya data za aina mbili, ambazo ni data za awali na data za upili ili kukamilisha malengo mahususi na kujibu maswali ya utafiti huu. Kwa hivyo mtafiti amebainisha aina za data alizokusanya kama ifuatavyo:

### 3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile data halisi ambazo hazijawahi kukusanywa na watafiti wengine kwa madhumuni ya kujibu maswali ya utafiti (Kothari, 2008). Data za msingi ni aina za data ambazo mtafiti huzikusanya kwa kutumia njia za mahojiano, usaili, uchunguzi makini na hojaji. Hizi ni data hai ambazo hazijawahi kukusanywa na mtafiti yeyote yule kwa lengo la kujibu maswala ya utafiti yaliyoulizwa na utafiti huo. Kitendo cha ukusanyaji wa data ni hatua mojawapo muhimu sana katika shughuli ya utafiti. Kabla ya kuanza kazi ya kukusanya data mtafiti hupaswa kujua ni aina gani za data anazohitaji kuzikusanya au ni kiasi gani cha upeo utakaomuwezesha kuamini kwamba data alizozikusanya zilitatosha kukidhi mahitaji yake na kukamilisha lengo lake la utafiti. Katika utafiti huu data za msingi zilihusu dhamira za lugha ya utani zinazozungumzwa katika masoko ya kuuzia samaki katika eneo la Kaskazini Pemba lililoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu.

### 3.6.2 Data za Upili

Panneerselven (2004) anasema data za upili ni aina za data ambazo tayari zimeshafanyiwa kazi, hivyo mtafiti hukusanya data hizo kutoka sehemu zilizoandikwa kama vile majarida, machapisho ya serekali, vitabu, utafiti na tasnifu. Kothari (2004) anafafanua kuwa data za upili ni zile ambazo zimekwishakusanywa na watafiti wengine na kuchapishwa ama kuandikwa. Hivyo basi ili kuzipata data hizo, mtafiti alilazimika kusoma machapisho tofauti katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania- tawi la Pemba, Maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Maktaba kuu Zanzibar –Maktaba zote ni tawi la Pemba. Mtafiti pia alipata data za aina hiyo kupitia na wavuti na wavu pepe. Kwa mnasaba huo, data za upili za utafiti huu zilihusu juu ya dhana nzima ya utani kutoka tafiti mbali mbali ikiwa ni sehemu mojawapo ya kazi tangulizi. Kwa ujumla Data za upili ni data zilizokusanywa kutoka tafiti nyengine ili kutoa msaada kwa mtafiti kufikia malengo na kujibu maswali kulingana na mada ya utafiti.

## 3.7 Mbinu za Kukusanyia Data

Opie (2004) anasema kwamba Mbinu za utafiti ni mipango inayowekwa katika kukusanya na kuchambua taarifa kwa kupata ukweli, ili kusuluhisha jambo, kujibu swali la utafiti au kutatua tatizo. Kwa hivyo mtafiti ametumia mbinu ya ushuhudiaji, mahojiano (usaili) kwa data za awali na mbinu ya upitiaji wa nyaraka kwa data za upili. Katika mbinu ya upitiaji wa nyaraka (machapisho) mtafiti alipitia machapisho mbali mbali yanayohusu utani na dhamira zinazopatikana kupitia utani huo. Aidha mtafiti ametumia mbinu ya ushuhudiaji katika kushiriki kama mtazamajiwa shughuli zinzotumia lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Kwa

upande wa mbinu ya mahojiano, mtafiti amewahoji watu 70 wanaume 49 na wanawake 21 katika sehemu husika za masoko ya kuuzia samaki.

### 3.7.1 Mbinu ya Ushuhudiaji

Ushuhudiaji ni mbinu ya kukusanya data ambayo hutumika kwa kuhudhuria katika baadhi ya sehemu zenye matukio halisi yanayohusianana mada inayofanyiwa utafiti na mtafiti akiwa kama mtazamaji (Omary, 2011). Ushuhudiaji ni mbinu mojawapo ya ukusanyaji wa data ambayo mtafiti wa kazi hii aliitumia katika utafiti wake. Mtafiti alilazimika kutumia mbinu hii ya kwenda katika maeneo husika na kushuhudia lugha ya utani ikitumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba na kushuhudia utani ukitumika.

### 3.7.2 Mbinu ya Usaili

Mbinu ya usaili ilitumika vyema katika utafiti huu kwa mnasaba wa kupata data za msingi za utafiti. Kothari (2013) anabainisha kuwa mbinu hii huwepesisha upatikanaji wa data kwasababu inawajumuisha wanaojua kusoma na wasiojua kusoma. Kombo na Tromp (2006) wanasema mahojiano ni mbinu za ukusanyaji data kwa njia za mazungumzo ya moja kwa moja baina ya mtafiti na watafitiwa. Aidha, husaidia kupata data muhimu zaidi kwa kutoa fursa zaidi kwa mtafiti kuuliza maswali ya ziada. Kwa hivyo mbinu ya mahojiano ilitumika katika utafiti huu ili kupata data za msingi za mada husika. Mtafiti alitumia mbinu hii kutokana na sababu kwamba alibaini mbinu hii huibuwa taarifa za siri ambazo mtafiti asingeweza kuzipata kwa kuzingatia watu wengi hupenda zaidi kuzungumza kuliko kuandika. Kadhalika, mtafiti ametumia mbinu hii kutokana na faida alizozibaini. Kwa mfano mtafitiwa anaweza kumuuliza mtafiti swali kama bado hajalifahamu na mtafiti

hupata fursa ya kutoa ufafanuzi kwa maswali yote ambayo yanakuwa na utata au magumu kueleweka. Pia mbinu hii hutoa fursa ya mtafiti na mtafitiwa kuweza kubadilishana mawazo mbalimbali yanayohusiana na mada husika.

### 3.7.3 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka

Mbinu ya upitiaji wa nyaraka imelenga kusoma, kuhakiki na kutalii kwa umakini kazi mbali mbali zenye uhusiano na mada husika. Upitiaji huo hutumika zaidi katika ukusanyaji wa data za upili za mada inayotafitiwa. Kwa mnasaba wa malengo na maswali na mada ya utafiti huu, mbinu ya upitiaji wa nyaraka imetumika kwa kukusanya data za upili zinazohusu utani. Maktaba mbalimbali zimetumika kama ndio msingi muhimu wa mbinu hiyo. Maktaba hizo ni pamoja na maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na maktaba kuu Zanzibar. Sambamba na hilo matumizi ya wavuti *(internet)* yametumika kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa data za utafiti huu vyema.

## 3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data za Utafiti

Wataalamu mbali mbali wameeleza kuhusiana na uchambuzi wa data za utafiti, miongoni mwao ni Bogdan na Biklen (1992) wakinukiliwa na Omary (2011) wanaeleza kuwa uchambuzi wa data ni hatua muhimu sana katika kutafuta majibu ya tatizo la utafiti husika. Kothari (2013) anasema uchambuzi wa data ni kitendo cha kuangalia na kufafanua vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo ilisaidia mtafit kujibu maswali ya utafiti husika. Utafiti huu umetumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo na mkabala wa Kitakwimu/Kimahesabu.

### 3.8 .1 Mbinu ya Mkabala wa Kimaelezo

Utafiti huu umetumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo kwa lengo la kupata uelewa na kubainisha dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Sababu kubwa iliyomsukuma mtafiti kutumia mbinu hii ni kwamba mbinu yenyewe inampa fursa na uwezo wa kuitumiaili kuweza kupanga data katika kundi moja linalofanana na kulingana na kuweza kuzitolea maelezo ya kutosha. Vile vile mtafiti ameona mbinu hii ni muwafaka zaidi kulingana na mada na malengo ya utafiti wake na kumuwezesha kujibu maswali ya utafiti wake na kutoa ufafanuzi wa kutosha. Hivyo basi utafiti huu umetumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo katika uchambuzi wa data za utafiti zinazohusu dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba.

### 3. 9 Maadili ya Utafiti

Neno maadili limejadiliwa kwa namna na mitazamo tofauti. Kothari (2013) ametaja baadhi ya maadili ya utafiti kuwa ni haki ya kuwa na siri, kwa maana ya kuwa mtafiti kwa namna yoyote ile anatakiwa asitowe siri ya mtafitiwa, pia anatakiwa kumuhakikishia usalama wake, mtafiti anahaki ya kutaka kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swala atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti. Kwa hivyo mtafiti alizingatia kwa kina kipengele cha maadili na kuweza kutunza siri pamoja na miiko yote inayohusiana na utafiti huu, wakati wa utafiti na hata baada ya matokeo ya utafiti. Kwa hivyo maadili ya utafiti ni utaratibu wa kuheshimu na kutekeleza zoezi zima la utafiti kwa kutofanya kinyume na sheria na taratibu za utafiti.

## 3.10 Hitimisho

Katika sura hii ya tatu mtafiti ameeleza mbinu na vipengele mbali mbali vya utafiti. Vipengele hivyo ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji. Pia, utafiti huu ni wa uwandani na hivyo mtafiti ametumia mbinu za ushuhudiaji na usaili katika kukusanya data. Katika sura hii pia kumewasilishwa vipengele vya mbinu za uchambuzi wa data, maadili ya utafiti na hitimisho.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti ambao umewasilishwa kwa kuzingatia malengo mahususi mawili ya utafiti huu. Lengo mahususi la kwanza lilihusu kuchambua dhamira za lugha za utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba na lengo la pili ni kubainisha mbinu za kisanaa za lugha ya utani inayotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba.

## 4.2 Dhamira za Lugha ya Utani katika Masoko ya kuuzia Samaki Kaskazini Pemba

Tumeanza kwa kubainisha aina za lugha ya utani unaofanyika katika masoko ya kuuzia samaki Pemba Kaskazini kwa kubainisha makundi matatu ambayo utani wa kimatendo, utani wa majina na utani wa kimisemo. Hii imefanya kazi ya uchambuzi wa data kuwa rahisi na yenye tija. Makundi hayo yamefafanuliwa kwa muhtasari katika jadweli lifuatalo:

**Jedwali 02: Muhtasari wa aina za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba**

| Na. | Utani wa Kimatendo | Utani wa Misemo | Utani wa Majina |
|---|---|---|---|
| 1 | Kusukumana | Kama umvuvi tutaonana mwambani | Kama umvuvi tutaonana mwambani |
| 2 | Kupigana | Tutaonana juu | Tutaonana juu |
| 3 | Kulipiwa mtu samaki na kuambiwa achukuwe bure | Chukuwa ukampe mke wetu | Chukuwa ukampe mke wetu |
| 4 | Kutiana matope | Haigwi | Haigwi |
| 5 | Kurushiana maji ya vumba | Goyalyo | Goyalyo |
| 6 | Kutia samaki mchanga na mwenyewe kuwafuta. | Matului (hayumo katika watakao uzwa) | Matului (hayumo katika watakao uzwa) |
| 7 | Kukonyezana | Nyegezo | Nyegezo |
| 8 | Kuoshwa miguu | Sukuma twende | Sukuma twende |
| 9 | Kununuliwa samaki | Kale na mkeo | Kale na mkeo |
| 10 | Kutia mchanga samaki | Kampe mke wetu | Kampe mke wetu |
| 11 | Kushikwa matako | Bwege | Bwege |
| 12 | Kushikana mashavu | Mshenzi | Mshenzi |
| 13 | Kushikana chuchu | Khanithi | Khanithi |
| 14 | Kutukanana | Nipe nikupe | Nipe nikupe |
| 15 | Kufichiana samaki | Msenge | Msenge |
| 16 | Kutia bei kwa ajili ya kukomoana | Mwehu | Mwehu |
| 17 | | Mwendawazimu | Mwendawazimu |
| 18 | | Kijiokazi | Kijiokazi |

Sambamba na makundi hayo, mtafiti amechambua Dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kwa kuhusisha na Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Dhamira ya Kujenga Umoja na Mshikamano

Silaha kubwa ya wanyonge katika jamii ni umoja na msikamano duniani kote. Dhamira hii imejitokeza katika utani unaofanyika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Utani katika masoko ya kuuzia samaki hufanywa kwa mantiki ya kujenga umoja na mshikamano kati ya wanajamii wanaohusika na shughuli za masoko hayo. Kuwepo na umoja na mshikamano katika jamii hiyo, hupelekea upendo katika shughuli zote za kijamii, kisiasa, kiutamaduni na hata kiuchumi. Mfano wa utani unaofuata unathibitisha hilo ni mtafiti kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji katika soko la kuuzia samaki la Tumbe, alibaini matendo ya baadhi ya watu, waliokuwa wakinyopora samaki wa wavuvi, wakati wakiwa kwenye mnada (mauzo). Unyoporaji huu hufanywa na baadhi ya watu ambao kwa makusudi huteuwa baadhi ya samaki na mara nyengine huwa ni wale samaki wakubwa. Wanyoporaji huwachukuwa samaki hao bila ya kuomba ridhaa kutoka kwa wavuvi ambao ndio wamiliki wa samaki hao. Hili linapotokea wenye samaki wanakuwa hawakasiriki. Tendo kama hilo ni dhahiri kwamba huonesha umoja na msikamano wa hali ya juu katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini kupitia soko la Tumbe. Utani wa aina hiyo ni wakipekee kwasababu katika hali ya kawaida tendo kama hilo haliwezi kulifanyika kwenye mazingira ya kawaida, watu wakatulia na kuvumilia.

Kimsingi, tendo hili linatufahamisha kwamba baadhi ya matendo ya kiutani yanayofanyika katika masoko ya kuuzia samaki hupelekea kuwepo na faida kubwa katika jamii hasa kwa wanaotaniana. Tendo kama hili linatoa mafunzo kwamba hata kama mwanajamii hana pesa za kununulia samaki katika masoko hayo anaweza kufaidika kupata samaki kupitia utani huo. Sharti la msingi kwake anatakiwa uwe ni miongoni mwa watani katika masoko hayo.

Kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kupitia muhimili wake unaohusu matini/kitendo husika kinaweza kuwa tofauti kwa namna kinavyoelekeza au kutatiza kwa mwitiko wa msomaji. Hii ina maana kwamba kitendo cha watu kuchukuwa samaki bila ya kuwashauri wahusika wenyewe ili kupata ridhaa zao, ni jambo ambalo linajenga mashirikiano miongoni mwao. Mambo hayo pamoja na kutokea maeneo ya masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba, kadhalika katika jamii zetu hujitokeza.

### 4.2.2 Dhamira ya Kuelimisha Jamii

Swala la elimu ni jambo muhimu sana kwa jamii yeyote inayohitaji maendeleo. Hii ni kwa sababu baadhi ya nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania swala la elimu bado halijapewa kipaumbele na umuhimu unaostahili. Kuna makundi mbalimbali katika jamii, ambayo yanastahiki kupatiwa elimu kwa mujibu wa amali zao lakini bado serikali haijaona haja ya kufanya hivyo. Vile vile utani unaofanyika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ni dhahiri unafunza na kuelimisha jamii. Kwa mnasaba huo wanajamii siku zote wanapaswa kujuwa kwamba popote wanapopatwa na tatizo la aina yoyote ni vyema kukimbilia kwa wanajamii wenzao kutafuta ushauri, nasaha na hata maelekezo bila ya kufanya hivyo tatizo lao linaweza lisitatuke na huenda likapelekea madhara makubwa baadae. Aidha utani unaofanyika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ni moja katika njia muhimu za kutolea elimu kwa jamii juu ya swala la kutunza na kuendeleza amali mbalimbali za jamii husika. Hali hiyo inajitokeza katika mfano ufuatao:

Mtafiti katika soko la kuuzia samaki lililopo Shumba Mjini Kaskazini Pemba kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji, aligundua baadhi ya watu wanasubiri wavuvi

bandarini. Wavuvi wanapofika na samaki wao na wakati mauzo yanaendelea watu hao huomba samaki kutoka kwa wavuvi hao. Pindi wavuvi wakiridhia kutoa walichoombwa, muombaji hutia mchanga baadhi ya samaki. Kwa utaratibu wa sokoni hapo samaki waliotiwa mchanga na mtu kwa makusudi wakati mauzo yanaendelea kama mchanga huo haukufutwa na mvuvi aliyeleta samaki wake, basi samaki hao katika mauzo hawahusiki. Mara tu baada ya mauzo kumaliza wanakuwa mali ya yule aliyetia mchanga bila ya kununuwa. Huo ni miongoni tu ya utani unaotumika sokoni hapo.

Hata hivyo, mtafiti ameshuhudia watu wengi ambao hukosea utaratibu huo kwa kujiamulia tu kutia mchanga samaki wa mvuvi bila ya hata mwenyewe kumwambia na kutaka ridhaa yake. Jambo hili hupelekea kuibuka kwa aibu kubwa ambayo inawakumba watu wa namna hiyo. Katika hali hiyo tunapata mafunzo makubwa na elimu ya kutosha kwamba tunapokuwa katika masoko ya kuuzia samaki tusijiamulie tu mambo kwa matakwa yetu katika samaki wa watu, isipokuwa tunatakiwa tufuate utaratibu ili tuweze kufanikiwa kirahisi katika mahitaji yetu.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo moja kati ya misingi yake ni kumpa uhuru mhakiki au msomaji, kuelewa na kuhakiki kazi ya fasihi kwa mtazamo na maoni yake mwenyewe, mtafiti ameweza kuzichunguza na kuzihakiki data za kifasihi alizozipata katika maeneo ya kuuzia samaki na kubaini kwamba kwenye utani unaotumika katika sehemu hizo dhamira ya kuelimisha hujitokeza katika njia mbalimbali. Mambo kama haya pia yanapatikana ndani ya jamii zetu pia. Kwa mfano, katika jamii ya Kipemba huweza kutokea babu akamnyang’anya mjukuu wake chakula na baadae akaondoka nacho. Lengo la msingi hapa si

kumkatili bali ni kutoa elimu kwa jamii juu ya swala la kutunza na kuendeleza amali mbalimbali za jamii husika ikiwa ni pamoja na kufanya kazi na kujenga uhusiano mwema miongoni mwa jamii.

### 4.2.3 Dhamira ya kuburudisha jamii

Mara nyingi utani hujengeka katika misingi ya kicheko au furaha ambayo kwa kawaida hutokea pale ambapo mtu amefurahishwa au amependezeshwa na jambo fulani. Matendo ya utani hutawaliwa na burudani na furaha. Hili ni jambo la msingi ambalo huwasababisha watu wanaofanya kazi katika maeneo ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kutaniana. Mfano, mtafiti kwa mnasaba wa data alizokusanya katika soko la kuuzia samaki lililopo Msuka Kaskazini Pemba kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji aligundua matendo ya baadhi ya watu kuwarushia watu maji machafu ya vumba la samaki ambayo kimsingi ni matendo ya kuudhi. Licha ya kuwa kitendo hicho kimsingi kinaudhi, lakini jambo hilo hupelekea kuibuwa vicheko na kuleta burudani kubwa kwa watu wanaofanya kazi katika eneo hilo la masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Katika hali ya kawaida matendo haya yanaonekana ni ya kishezi na kipuuzi na yasiyo na heshima, lakini katika uhalisia wake matendo hayo ni fani ya fasihi inayotumika katika sehemu za masoko ya kuuzia samaki. Fani hizo kama zilivyo fani nyengine za kifasihi hulenga kuibua burudani ndani yake. Burudani hizi hupelekea watu wakubwa kulia hadharani. Wakati jamii siku zote inaamini kilio kwa watu wazima kinatokana na majanga au huzuni, lakini kwa mazingira ya utani unaotumika katika masoko ya kuuzia samaki hii huonekana kuwa ni sehemu ya burudani kubwa. Kilio cha mtu mzima kwenye maeneo haya si alama ya majanga kwasababu miongoni mwa watu katika sehemu hizo za sokoni hujawa na

furaha na kujikutia wanalia huku wakitokwa na machozi ya furaha, bila ya hata kuwepo na majanga yoyote. Hali hii ikitokezea sehemu nyengine yoyote kinyume na sehemu hizo watu hukasirika, kuondosheana haiba, staha na hata kufikishana katika vyombo mbali mbali vya kisheria ikiwemo polisi.

Kwa mujibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika msingi wake unaosema kuhusu vipengele vya kimsingi ambavyo huunda Mwitiko wa Msomaji. Mtafiti kwa kuongozwa na muhimili huu, amepata uthubutu wa kusema kwamba kitendo kilichotumika cha kurushiana maji machafu au maji ya vumba la samaki ni katika baadhi ya kuimarisha utani miongoni mwao. Kwa muktadha wa jamii ya watu wa eneo hilo vitendo hivyo si vitendo vya kuudhi bali ni vitendo vya kuburudisha na kuleta burudani kwa jamii husika.

### 4.2.4 Dhamira ya ustahamilivu katika kazi

Ustahamilivu katika maisha ni jambo linalofaa katika maisha ya mwanadamu. Mwanaadamu anatakiwa astahamili ili aweza kuhimili mikiki na majanga mbali mbali ambayo yanaweza kumkabili katika shughuli zote za kijamii katika maisha ya kila siku. Ukweli wa maelezo haya unadhihirika zaidi katika baadhi ya matendo ya lugha za utani yanavyofanyika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kama ifuatavyo:

Katika soko la kuuzia samaki lililopo Kojani, kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji mtafiti amebaini kujitokeza matendo mbali mbali ya kimaudhi kama vile, iwapo mtu anataka kununuwa samaki na akajitokeza mtu mwengine kununuwa samaki wale au wengine basi yule aliyefanikiwa kununua mwanzo humwambia mwenzake,

"*samaki hawa kampe mkeo na umwambie leo ajipambe vizuri mimi leo nakuja kulala huko".* Suala kama hili kwa watu wa jamii ya Kipemba hupelekea kuibuka kwa maudhi makubwa ambayo yanaweza kusababisha ugomvi ndani yake. Kwa sababu hiyo, utafiti huu umegundua ni bora mtu wa Pemba kumtukana yeye binafsi haumii sana kuliko kumtajia mke wake, hasa katika sehemu hizo za mikusanyiko ya watu kama vile masokoni. Lakini kutokana na mila na desturi zinazotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba, akijuwa kwamba ni moja kati ya utani wao unaotumika katika sehemu hizo, mtu anakuwa mstahamilivu na kuvumilia maudhi yote dhidi yake.

Kwa kurejelea katika nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika msingi wake unaompa uhuru msomaji/mhakiki kuiangalia matini ya kazi ya fasihi kwa jinsi anavyoiona msomaji /mhakiki, hivyo basi mtafiti alipochambua baadhi ya misemo kama vile *sukuma twende*, *goyalo, kama mvuvi wa pweza tutakutana mwambani* inayotumika katika masoko ya kuuzia samaki alibaini kuwa misemo kama hiyo inawajenga watu kuwa wastahamilivu katika jamiii, katika harakati za kukabiliana na mambo mbalimbali ya kijamii. Mtafiti amelazimika kusema hivyo kwasababu swala la kumuhonga mtu samaki na kuambiwa akampe mkewe, na halafu yule aliyehongwa samaki akaagizwa amwambie mkewe ajipambe vizuri kwani mtoa samaki atakuja kulala badala ya mwenye mke, ni jambo gumu linalohitaji ustahamilivu wa hali ya juu.

### 4.2.5 Dhamira ya kujenga ujasiri

Suala la ujasiri ni suala linalompa mtu heshima kubwa kwa jamii iliyomzunguka. Heshima hupatikana pale ambapo mtu au jamii hukumbwa na kadhia yoyote ambayo

katika hali halisi inahitaji mapambano ya aina yoyote katika nafsi ya aliyetatizika ili kuweza kujikwamua na hali hiyo. Suala kama hilo hujitokeza sana katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kwa mtu au watu kukumbwa na kadhia kubwa kwa matendo yanayojitokeza dhidi yao na kupaswa kutumia ujasiri wa hali ya juu kuweza kujikwamua na hali hiyo. Mfano wa matendo yanayofuata yanaweza kutudhihirishia ukweli huo:

Mtafiti katika soko la kuuzia samaki lililoko Tumbe Kaskazini Pemba, kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji aligundua matendo ya watu wa kiume kukamatwa mashavu, chuchu na kukamatwa matako na wanaume wenzao pamoja na kuambiwa maneno yanayoonyesha dharau na kejeli ikiwa ni sehemu ya utani. Maneno wanayoambiwa ni kama vile, mjinga, bwege, khanithi na mengine yanayolingana na hayo. Matendo na maneno kama haya katika hali halisi ni makubwa na ya kuudhi sana na hayapendezi. Mtu akiweza kuyavumilia huweza kuitwa jasiri. Anaweza kuitwa jasiri kwa sababu matendo na maneno hayo hufanyika mbele za watu wengi wakiwamo wake na waume, wakubwa na wadogo, ambapo wenye kufanyiwa hukasirika na kughadhibika sana. Mtafiti ameshuhudia baadhi ya wavuvi wakifanyiwa matendo na kuambiwa maneno kama hayo na huku wakiweza kudhibiti hasira zao na wala hawakuchukuwa hatua yoyote. Hali hiyo mtafiti ameiita ni ya kijasiri kwa sababu sehemu nyengine zozote si aghalabu kwa mtu mzima kufanyiwa vitendo vya namna hiyo bila ya kukasirika na kuchukuwa hatua za kisheria.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika muhimili wake unaosema Maana ya kazi yoyote ya kifasihi inamtegemea kwa kiasi kikubwa mhakiki/msomaji wa kazi hiyo. Hii ina maana kuwa ni vigumu kudai au hata kusema kuwa kuna

maana fulani sawa na sahihi ya kazi fulani ya kifasihi kwa msomaji. Mtafiti katika kuchambua data zake alipata nafasi ya kuhakiki matendo na maneno ya utani ya watu kukamatwa mashavu, chuchu au matako na kuambiwa maneno machafu bila ya kukasirika na kuchukuwa hatua na kuweza kustahamili kwa maudhi hayo kwamba ni kitendo cha ujasiri. Mtafiti kitendo na maneno kama haya ameyaita ya ujasiri kwasababu matendo na maneno hayo kama mtu hana ujasiri asingeweza kabisa kuvumilia. Hata hivyo, mtafiti wa kazi hii amebaini kwamba ndani ya jamii zetu matendo na maneno kama hayo yanaweza kujitokeza. Tajiriba alizonazo na uzoefu wake wa maisha umemuwezesha mtafiti kuyashuhudia mengi yanayohusu ujasiri wa aina hii. Mtafiti ametoa mfano kwa kusema kwamba katika jamii ya Wapemba anaweza kushuhudiwa babu au bibi anafanyiwa karaha na mjukuu wake kwa kushikwa matako au maziwa na kuambiwa maneno ya kipumbavu. Babu au bibi huyo akaweza kustahamili maudhi hayo, kwasababu anaelewa kwamba ni katika sehemu tu ya maisha yao ambayo yamejengeka katika misingi ya kiutani.

### 4.2.6 Dhamira ya ukakamavu katika kazi

Suala la ukakamavu katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ni la lazima. Suali kama hilo linampasa kila mtu katika sehemu hizo awe nalo. Hili linajengwa na matendo ya kiutani yanayojitokeza mara kwa mara katika harakati za kujitafutia mahitaji ili yaweze kumvuusha vyema mwanajamii katika maisha ya kila siku. Katika kulidhihirisha hili ni busara kuangalia mifano ya baadhi ya matendo na maneno ya utani yanayojitokeza katika masoko ya kuuzia samaki ambayo hupelekea kuwepo kwa ukakamavu:

Suala la watu kupigana na kutoleana maneno machafu katika masoko, hujitokeza siku hadi siku ambapo ni miongoni mwa utani wao unaotumika sehemu hizo kwa wale watu wanaotaniana. Mtafiti katika harakati za kukusanya data kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji ameshuhudia watu wakipigana na kutoleana maneno machafu katika soko la kuuzia samaki lililopo Wete. Bila sababu utaona watu wakisukumana wala sio kwamba wamekasirikiana au kuchukiana, isipokuwa ni katika misingi ya kuendeleza utamaduni wao wa utani. Maneno hayo wakati mwengine huambatana na maneno ya matusi. Watu wengi katika mazingira hayo walikuwepo na huku wakiwa wanashangilia kwa maneno ya mzaha na kucheka bila ya hata kuamuwa ugomvi uliokuwa ukiendelea. Mara baada ya mapigano hayo watu hao walijiamua wenyewe wakawa wanacheka na kukumbatiana. Hakuna hata mmoja miongoni mwao aliyediriki kuchukuwa hatua za kisheria. Matendo na maneno hayo yanatufahamisha na kutuelekeza wazi wazi kwamba katika utani unaofanyika sehemu za masoko hayo kunahitajika kuwepo na ukakamavu wa hali ya juu wa kimwili ili mtu aweze kukabiliana na kupambana na hali yoyote itakayoweza kujitokeza sokoni hapo.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika muhimili wake unaompa fursa mtafiti huihakika kazi ya fasihi kutokana na mtazamo wake, mtafiti huku akiongozwa na muhimili huu ametafsiri kwamba yale matendo na maneno ya utani ya kupigana kusukumana na kuambizana maneno yasiofaayanayojitokeza katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba si katika matendo ya kikatili au kihuni isipokuwa ni matendo ambayo humjenga mtu kuwa mkakamavu.

### 4.2.7 Dhamira ya kuhimiza jamii katika kazi

Kuhimizana katika kutenda jambo jema ni kitendo kinachoharakisha kupatikana kwa maendeleo katika jamii. Hali ya kuhimizana hujitokeza siku hadi siku katika

mazingira ya jamii kwa mnasaba wa kujiharakishia mahitaji ya kila siku. Matendo ya huhimizana hujitokeza pia katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ikiwa ni moja kati ya matendo ya kiutani. Mfano ufuatao unalidhihrisha hili:

Katika soko la kuuzia samaki lililoko Kojani hujitokeza vitendo vya watu wa kiume ambao ni wanunuzi na waombaji wa samaki kutia mchanga au kukata mkia samaki wa watu ambao wameletwa sokoni kwa ajili ya mauzo. Matokeo hayo hujitokeza bila ya hata ruhusa kutoka kwa wenye samaki hao. Kwa mujibu wa desturi za sehemu hizo, samaki wakitiwa mchanga au kukatwa mkia kama hawakufutwa mchanga huo, au kukataliwa kukatwa mkia samaki hao, mara baada ya mauzo samaki wale wanachukuliwa ni yule mtu aliyetia mchanga huo au aliyewakata mkia. Mtiaji mchanga au mkataji mkia wa zamaki anajimilikisha samaki hao bila kutoa gharama yoyotekma malipo. Tendo hilo hufanyika kwa maridhiano baina ya mvuvi na mtiaji mchanga kwenye samaki. Iwapo mvuvi hakuridhika na utaratibu huo hukasirika na kutoa maneno huku akiwafuta mchanga samaki wale kwa hasira na huku akiwa anassema maneno makali mno na huku akisema, “kama mtu anahitaji samaki aende akavuwe wake, halafu aje aachie watu wateuwe samaki wazuri wawatie mchanga au wakate mkia.” Katika mazingira kama hayo ni dhahiri kwamba katika utani huo tunapata mafunzo ya kuhimizwa kufanya kazi. Tunakatazwa kuwa wavivu na kuhitaji kupata vitu kirahisi rahisi. Tunatakiwa tuende tukajitume ili tuone uchungu wa mtu kuchukuliwa mali yake bure.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika mtazamo wake usemao kwamba, matini husika inaweza kuwa tofauti kwa namna inavyoelekeza au kutatiza mwitiko wa msomaji. Sifa ambayo huonesha uhakiki mzuri au uhakiki mbaya kwa

kazi inayohusika. Mtafiti kwa kuongozwa na mtazamo huu, ameona tabia hii inafaa kuendelezwa kama sehemu ya kulinda utamaduni wa kiutani maadamu hauna dhamira ya kusababisha madhara. Kitendo cha mwenye samaki kukasirika na kufuta mchanga samaki wake na huku akiwa anasema kwa ukali, kama mtu anataka samaki na aende akavue wake halafu aje aachie watu wachukuwe ni kitendo ambacho kina mafunzo ndani yake. Kitendo hiki kinatuhimiza kwamba mwanadamu siku zote anatakiwa kujituma na kufanya kazi kwa nguvu zake zote ili kujipatia kipato halali, na sio kukaa tu bila ya kufanya kazi na kufuga uvivu huku wakiwa wanasubiri vitu vya watu wengine.

### 4.2. 8 Dhamira ya kuwa na upendo katika kazi

Upendo katika maisha ya binadamu ni jambo zuri na linalopaswa kuendelezwa katika jamii zote ulimwenguni. Binaadamu anastahiki upendo ili kumwezesha kuishi katika raha na starehe katika harakati zake za kimaisha. Katika sehemu za masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba suala hili la upendo linakuwepo na kushamiri siku hadi siku. Upendo huu unasababishwa na matendo ya kiutani yanayotumika katika sehemu hizo za masoko ya kuuzia samaki kwa mnasaba wa kujifurahisha, kujiliwaza na kujipa matumaini katika biashara zao. Mfano unaofuata unadhihirisha ukweli huo:

Katika soko la kuuzia samaki lililoko Kojani Kaskazini Pemba hujitokeza matendo ya watu kununuwa samaki na kuwapa watani wao, hukuwakiwaambia kwamba, samaki hawa kampe mkeo ale na watoto wetu. Tendo kama hilo huonesha upendo wa hali ya juu baina yao, kwasababu katika hali ya kawaida sio kitu rahisi kwa watu wanaofanya shuhghuli zao katika maeneo mengine yasiyokuwa haya kuweza kufanya hivyo kwa mnasaba wa kuonesha upendo kati yao. Kawaida ya moyo wa

mwanadamu hujenga upendo kwa mtu aliyemtendea wema. Hali hii ya mtu kununuliwa samaki na kuambiwa kale na watoto wetu huibuwa upendo miongoni mwao.

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kupita muhimili wake usemao Maana ya kazi yoyote ya kifasihi inamtegemea kwa kiasi kikubwa cha mhakiki/msomaji wa kazi hiyo, umetumiwa na mtafiti kuhakiki matendo na maneno ya kiutani yanayotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Mfano na matendo kama hayo ni yale ya mtu kupewa samaki na kuambiwa nenda kale na watoto wetu na kubaini kwamba ni matendo ambayo hujenga upendo kati yao.

### 4.2.9 Dhamira ya kuonya jamii

Utani unaofanyika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba unatupa dhamira ya kuonya jamii kwa lengo la kukuza maadili na kuishi kwa amani. Mtafiti ametuonesha na kutufahamisha kwamba watu wanapoondoka majumbani kwao kuenda kwenye masoko ya kuuzia samaki ni vyema kuwa na mahitaji yao ya kutosha (pesa) kwasababu bila ya kufanya hivyo kunaweza kujitokeza vitendo vinavyopelekea kuwaadhirisha na kuwafedhehesha. Hapa jamii inafahamishwa kuwa utu wa mtu ni kazi.

Mtafiti ameyabainisha hayo katika matendo mbali mbali aliyoyashuhudia kwenye masoko ya kuuzia samaki kwa mfano, kwenye soko la Msuka kuna watu ambao shughuli zao kuu ni kutengeneza au kupara samaki, basi hutokea muda mwengine wakaiba baadhi ya samaki waliopewa. Njama hiyo inapogundulikana wenye samaki hukasirika na kuchukizwa sana kwa kitendo hicho, huku wakiwa wanamwambia mtu

huyo “Najua ulichukuwa samaki wangu lakini nenda ukale na mke wetu, ila ujuwe mtoto atakaezaliwa kwako ni wangu, wee samaki chukuwa lakini pesa hupati”. Hivyo jamii inaonywa ifanye kazi kwa uaminifu na kuachana kabisa na tabia ya wizi.

Kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa msomaji katika muhimili wake unaosema Matini husika inaweza kuwa tofauti kwa namna inavyoelekeza au kutatiza kwa mwitiko wa msomaji. Kwa kuongozwa na muhimili huu wa nadharia ya Mwitiko wa msomaji, mtafiti kumemuongoza kutafsiri matendo ya mtu kufanya kazi za kupara samaki na kunyimwa haki yake kwa sababu ya wizi, kwamba ni kuibuka kwa tabia mbaya na kutoa onyo kwa mwanadamu siku zote anatakiwa kujituma ili aweze kupata mahitaji yake ya kihalali na siyo kusubiri tu vitu vya watu na kuiba. Dhamira ya utani uliowasilishwa hapo juu ni kukemea vitendo vya wizi na ulagha, ambavyo havifai kuendelezwa na kubaki katika jamii.

### 4.2.10 Dhamira ya mmong’onyoko wa maadili

Msanii siku zote anapotunga kazi yake ya kisanaa sio kama anaichukulia ombwe tu linalotokana na fikra zake au hisia zake, bali kinatokana na jamii inayomzunguka. Hali hii hujitokeza wazi wazi katika utani unaofanyika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kama tunavyoona mfano ufuatao:

Mtafiti katika soko la kuuzia samaki lililoko Shumba ya mjini Kaskazini Pemba, kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji amebaini matendo ya watu kujikusanya sehemu moja kwa ajili ya kusikiliza mnada wa samaki. Mara nyingi watu huwa hukaa katika hali ya duara ambapo takribani huwa watu wa rika tofauti kati ya miaka 20 hadi 40 ambao ni vijana na kati ya miaka 50 hadi 70 ambao ni wazee na ndani yake wana

kuwepo na watoto wao pia. Katika mazingira kama hayo hujitokeza mmoja miongoni mwao hata kama ni mdogo akawasukuma watu wale na kuwaangusha chini bila ya kujali athari ambayo inaweza kujitokeza baadae. Kitendo cha kuwasukuma watu hufanyika kwa lengo la kujiburudisha. Hata hivyo, kitendo hicho ni kinyume na maadili ya Kizanzibari. Wakati mwengine watu hutokezea kukaa uchi kutokana na hali hiyo ya namna ya uvaaji wao wa nguo usio mzuri wakiwa sokoni hapo. Kwa sababu mara nyingi watu hao wanavaa nguo ambazo ni mapindi pindi na hili linatokana na maumbile na mazingira ya kazi wenyewe.

Kwa mnasaba wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika muhimili wake unaosema: Maana ya kazi yoyote ya kifasihi inamtegemea kwa kiasi kikubwa cha mhakiki/msomaji wa kazi hiyo, hii ina maana kuwa ni vigumu kudai au hata kusema kuwa kuna maana fulani sawa na sahihi ya kazi fulani ya kifasihi kwa msomaji. Mtafiti kwa kuongozwa na muhimili wa nadharia hii amepata fursa ya kueleza kwenyeukuhakiki kwamba, matendo hayo ya watu kusukumana na kuangushana yana lengo kuendeleza, kukuza na mila na kujenga uhusiano mwema pamoja na kuleta burudani katika kazi.

### 4.2.11 Dhamira ya utamaduni katika jamii

Utamaduni kuwa ni mila, jadi na desturi za kundi fulani katika jamii yoyote ile. Hivyo ni wazi kwamba utamaduni ni muhimili muhimu katika maisha ya jamii na ni kitambulisho cha jamii na taifa kwa ujumla. Utamaduni siku zote hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi chengine katika kukuza mila na desturi za jamii husika. Kwa msingi huo, katika utamaduni wa Mswahili swala la utani linachukuwa nafasi kubwa kama ilivyo katika jamii takribani zote ulimwenguni. Jamii nyingi katika mwambao

wa Afrika Mashariki watu kuishi pamoja, kushirikiana, kusaidiana na kutaniana huonekana ni jambo la kawaida ambapo ni moja kati ya utamaduni wao. Lugha ya jamii inayotumika huonekana ni sehemu ya utamaduni katika jamii husika. Matendo ya utani yanayotumika katika jamii hizo huonekana ni moja kati ya sehemu za utamaduni wa Waswahili. Katika hali ya namna hiyo ni dhahiri kwamba lugha inayotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ni moja kati ya utamaduni wa Waswahili kisiwani Pemba.

Mtafiti kwa kutumia mbinu ya dodoso amegundua kuwa utani unaotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba unaakisi hali halisi ya ya maisha na utamaduni wa Wapemba katika sehemu husika. Dhana hii hudhihirika katika matendo mbali mbali ya kiutani yanayotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ikiwa ni moja kati ya utani wao kama ifuatavyo:

Katika soko la kuuzia samaki Kaskazini Pemba lililoko Kojani, mtafiti kwa kuongozwa na mbinu ya ushuhudiaji ameona watu ambao shughuli yao kuu ni kupara na kutengeneza samaki waliokwishanunuliwa kama njia yao kuu ya kujipatia kipato. Katika shughuli hiyo hujitokeza watani na na kuwakejeli kwa kuwaita waparaji wa samaki, "*we dada, au we shangazi; hebu harakisha kutengeneza samaki wa muumeo hao.*" Mtafiti alibaini kwamba kitendo cha kumuita mwanamme dada au shangazi si lugha ya kawaida inayokwenda sambamba na utamaduni wetu wa Kipemba na jamii za Kizanzibari kwa jumla. Hata hivyo, kitu kikubwa cha kushangaza hapa ni lugha ambayo hutumika kuwakejeli wale waliojitokeza kujitolea katika kupara samaki lakini hawakasiriki wala kuhamaki. Huu ndiyo utani wenyewe

lakini kwa sababu ya utamaduni huo kuwa umezoeleka katika jamii watu wahakasiriki na huona kuwa ni utani tu.

### 4.2.12 Dhamira ya ukombozi

Kwa mujibu wa Abdalla (2018) ukombozi ni kitendo cha kubadilika kutoka katika hali duni ya maisha na kuingia katika hali nzuri ya maisha, katika nyanja mbali mbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa ujumla, ukombozi ni hali ya mabadiliko kutoka hali duni na kuelekea hali nzuri, inayompelekea mtu kuishi maisha yake kwa kadri anavyopenda. Katika kuchunguza dhana ya utani unaotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba, kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji, mtafiti amebaini kwamba dhamira ya ukombozi hujitokeza katika masoko mbali mbali ya kuuzia samaki yaliyopo Kaskazini Pemba.

Ukombozi wa kifikra umeonekana kushamiri takribani katika masoko yote ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Mtafiti aliyabaini na kuona watu mbali mbali wakitowa nasaha na ushauri juu ya watu kujitafutia kipato. Katika soko la Shumba ya Mjini Kaskazini Pemba, jambo hili lilibainika kwa kushuhdia kitendo cha dalali mmoja aitwae “Mtawa” alipomwambia kijana mmoja itwae “Kijee” kwamba ukija hapa sokoni usijikalie tu burebure utakumbwa na hali ngumu za kimaisha. Mtawa alimshauri Kijee kwenda kununua tenga halafu akija hapo sokoni awafuate wavuvi wanaorudi kuvua samaki uwaombe wale samaki awaingize kwenye tenga lake na halafu awabebe na kuwapelekea hapo sokoni kwenye mnada kwa ajili ya mauzo. Kwa kufanya hivyo *“Ndugu Kijee”* alijikutia baada ya siku chache amekuwa maarufu na hatimaye kujipatia kipato kizuri.

Kwa hakika mtafiti kwa kuongozwa na mbinu ya dodoso amegundua kwamba vitendo vile vya watu kupewa nasaha na ushauri juu ya kujikwamua na hali ngumu ya kimaisha, kama alivyofanya dalali "Mtawa" kumshauri "Kijee" kununuwa tenga na kuwafuata wavuvi ili waingize samaki wao na yeye kuwachukuwa na kuwapelekea mnadani kwa ajili ya mauzo. Ingawa maneno hayo yalitumika katika hali ya kiutani, lakini ndani yake yalikuwa na ukweli usio na shaka. Huu kwa hakika ni mfano mzuri ambao umetuonesha jinsi utani ufanywao kwenye masoko ya kuuzia samaki unavyoweza kuleta ukombozi wa kifikra kwa vijana.

Vile vile mtafiti amebaini swala la ukombozi wa kiuchumi likishamiri katika soko la kuuzia samaki lililopo Tumbe. Kwa kawaida kiwango kidogo cha fedha ya wastani shilingi elfu tano 5,000/= kwenye bei ya shilingi laki moja 100,000/= huchukuliwa na kuhifadhiwa na dalali anayehusika wakati wa mauzo. Siku ambazo wavuvi wanaouza samaki kwa kutumia dalali huyu wanataka mahitaji ya kiuvuvi kama vile pesa za kununulia mitego, na baadhi ya mahitaji mengine kama vile ukarabati wa chombo iwe rahisi kupata fedha kupitia kwa dalali huyo. Kwa kawaida katika mazingira ya masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba, dalali ndiye mwenye majukumu ya kununuwa na kutoa mahitaji madogo madogo katika chombo cha uvuvi. Pale wavuvi wanapohitaji fedha kutoka kwa dalali kwa dalali huyo, hujibiwa kwa lugha ya utani kwamba "*munakuja kuniomba pesa, kwani mimi ni mume wenu au mimi ndiye tajiri wenu, si mungalikwenda tuu kwa dalali wenu, 'Kome' awape hayo mahitaji yenu.*" Pamoja na utani huu lakini wavuvi hupatiwa fedha na kutimiza majukumu yao na kujikwamua kiuchumi.

### 4.2.13 Dhamira ya Ukweli na Uwazi

Ukweli na uwazi kwamba ni hali ya mtu kusema neno au kufanya jambo kama lilivyo bila ya kuficha kitu, au kuona aibu yoyote kuhusiana na jambo hilo. Dhana ya ukweli na uwazi ni moja kati ya matendo muhimu ambayo hutumika siku hadi siku katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Kwa mfano, katika soko la kuuzia samaki la Tumbe Kaskazini Pemba, mtafiti alibaini wavuvi wakichukuliwa samaki wao na mmoja kati ya watu mashuhuri waliopo sokoni hapo ambao hujiita wazee wa soko. Wavuvi walionesha kutoridhia kitendo cha mzee wa soko kuchukuwa samaki. Kutokana na kitendo cha kuchukuliwa samaki hao bure nahodha alidiriki kueleza bayana yaliyomo moyoni mwake kwamba mtu yoyote “aliyekuwa hana pesa asichukuwe samaki.” Hata hivyo, samaki walichukuliwa na kitendo cha kuchukuliwa samaki hao kilimfanya nahodha huyo akasirike sana lakini kwa sababu ni utani hakuwa na cha kufanya.

**Jadweli namba 03: Muhtasari wa dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba**

| Nambari | Dhamira za Lugha ya Utani | Maelezo |
|---|---|---|
| i) | Dhamira ya Kujenga Umoja na Mshikamano | √ |
| ii) | Dhamira ya Kuelimisha Jamii | √ |
| iii) | Dhamira ya Kuburudisha Jamii | √ |
| iv) | Dhamira ya Ustahamilivu katika Kazi | √ |
| v) | Dhamira ya Kujenga Ujasiri | √ |
| vi) | Dhamira ya Ukakamavu katika Kazi | √ |
| vii) | Dhamira ya Kuihimiza Jamii katika Kazi | √ |
| viii) | Dhamira ya Kuwa na Upendo katika Kazi | √ |
| ix) | Dhamira ya Kuonya Jamii | √ |
| x) | Dhamira ya Mmong'onyoko wa Maadili | √ |
| xi) | Dhamira ya Utamaduni katika Jamii | √ |
| xii) | Dhamira ya Ukombozi | √ |
| xiii) | Dhamira ya Ukweli na Uwazi | √ |
| | **Jumla** | **13** |

(Chanzo, mtafiti 2022)

### 4.3 Mbinu za Kisanaa za Lugha ya Utani

Wamitila (2002) anaeleza kwamba fani ni ufundi wa kisanaa unaotumiwa na mtunzi wa kazi ya kifasihi katika kuisana kazi yake. Akaendelea kusema ufundi huu wa kisanaa unapatikana katika vipengele vya matumizi ya lugha, wahusika, mtindo, muundo na mandhari katika kazi ya kifasihi. Kwa ujumla mtafiti anaona kuwa mbinu za kisanaa ni usitadi wa hali ya juu uliomo ndani ya kazi za kifasihi ambao huiwezesha kazi husika kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyolengwa. Miongoni mwa mbinu za kisanaa zinazojitokeza katika utani ni pamoja na matumizi ya

tashibiha, taswira, takriri, ishara, kejeli, misemo, majazi, methali na matumizi ya tashititi.

### 4.3.1 Matumizi ya Tashibiha

Tashibiha ni mbinu ya kisanaa ambayo hulinganisha vitu viwili kwa mshabaha kana kwamba vinafanana kabisa na hali ya kuwa ni tofauti. Miongoni mwa vipengele ama maneno ya mshabaha ambayo hutumika ni "kama vile, mithili ya, sawa na, kama na, na mengineyo." Katika soko la kuuzia samaki lililoko Tumbe, mtafiti alibaini matumizi ya tashibiha "*Mtizame anafanya kichwa na pembe kama ng'ombe wa pwani.*" Hapa kuna matumizi ya tashibiha ambapo binadamu anatajwa kichwa chake kuwa kinafanana na cha ng'ombe.

Kadhalika wakati wa kukusanya data mtafiti alipokwenda katika soko la kuuzia samaki lililopo Wete alibaini wanunuzi wa samaki (wachuuzi) wakisema kwamba katika bahari ya Msuka alikamatwa *"papa alikuwa mkubwa kama mbuyu".* Katika hali ya namna hiyo ni dhahiri ya kwamba kuna matumizi makubwa ya tashibiha ambayo yametumika katika maongezi haya. Paapa ni aina ya samaki ambae anapatikana baharini lakini mbuyu ni aina ya mti mkubwa ambao unapatikana aridhini na ambao kimaumbile ni mkubwa. Mti huo umeweza kufananishwa na jamii hiyo ya samaki ambae pia kimaumbile yake mara nyingi huwa ni mkubwa. Sifa nasibishi zilizofanya viwili hivi kufananishwa ni ukubwa. Unasibishi huu umefanyika kwa kutumia nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa Kiseme ambao hueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambapo hutupatia picha ya muhusika fulani wa kifasihi. Elementi nasibishi zilizosababisha kutumika tashibiha ni kiwango

cha unene na ukubwa wa papa ambacho ingawa kwa njia ya kuingiza chumvi kimefananishwa na papa.

### 4.3.2 Matumizi ya Taswira

Senkoro (2011) anasema kuwa taswira ni lugha inayochora picha ya vitu au mahali kwa kutumia ishara. Taswira ni mkusanyiko wa picha mbali mbali zinazoundwa na maelezo ya wasanii katika kazi za kifasihi. Naye Jilala (2016) anailezea mbinu ya taswira kwamba hurejelea matumizi ya lugha inayopambanuliwa na uteuzi mzuri wa maneno, ulinganifu na udhahiri wa maelezo yenye kuhusisha na kujumuisha dhana tofauti ili kuleta taswira au athari maalumu katika mawazo ya msomaji au msikilizaji. Kwa mfano, katika lugha ya utani inayotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba mtafiti amebaini matumizi ya lugha ya taswira "*akienda dukani kununua mfuko kwa ajili ya kutilia samaki wake, lakini ghafla alitokea mtani wake ambaye alikuwa ni mwanamke na kumwambia arejeshe ule mfuko na baadae yeye atampa mfuko ahifadhie samaki wake*." Mara baada ya kumuuliza uko wapi huo mfuko? Yule binti akamuonesha kwa kutumia kidole chake sehemu ya utupu wake wa mbele na kumwambia "*Wewe hao samaki wako wote njoo utie hapa. Unakwenda kutafuta mfuko wanini wakati mimi ninao huu hapa.*" Hapa kuna matumizi ya lugha ya taswira ambapo kinachoelezwa hapa ni utani lakini ndani yake kunajengwa taswira kwamba muuza samaki akishapata fedha baada ya kuuza samaki basi anaweza kutoa sehemu na kumpatia binti huyo ili na yeye muuza samaki apewe mapenzi.

### 4.3.3 Matumizi ya Takriri

Jilala (2016) anaitafsiri takriri kwa kusema kuwa huu ni mtindo wa usemi ambao msemaji hutumia neno au maneno kwa kurudiarudia kwa lengo la kutilia mkazo au kusisitiza jambo. Watumiaji wa lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba hutumia takriri katika mawasiliano na utani. Kwa mfano, wakati wa mauzo ya samaki dalali husema "shilingi elfu moja," watu wengine ambao ni wanunuzi husema "*tano, tano,*" na anapoendelea kutaja bei zaidi watu hurudiarudia vile vile "*tano, tano,*" mpaka mwisho wa bei ya mauzo ya samaki.

### 4.3.4 Matumizi ya Ishara

Jilala (2016) anasema kuwa, maneno kama vile taa na mwenge, hutumika kuwakilisha utambuzi, ujuzi au inaweza kuwa na msingi wa kitaashira kama vile kaburi, fuvu, jeneza ambavyo hutumika kuwakilisha mauti. Katika lugha ya utani inayotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba watumiaji hutumia lugha hii ya ishara katika nyanja mbalimbali kama vile kukonyeza na kutikisa kichwa. Watu mbali mbali ambao ni wanunuzi hutia bei zao kwa dhahiri na kusikika. Pia hujitokeza wanunuzi wengine wa samaki miongoni mwao wakawa wanatia bei zao kwa njia ya ishara kwa kukonyeza au kutikisha kichwa kuashiria kukubali au kukataa (kutikisha kichwa juu na chini kunaashiria kukubali. Kutikisha kichwa kulia na kushoto kunaashiria kukataa). Katika hali hiyo, mtafiti ameona kufanya hivyo upo ukweli usio na shaka kutumika matumizi ya kiishara katika sehemu hiyo.

### 4.3.5 Matumizi ya Kejeli

Mtafiti ameifafanua Kejeli kwa kusema ni usemi ambao maana yake ya ndani ni kinyume chake na inabeuwa maana yake halisi. Vile vile kejeli ni usemi wa kebehi

ambao kisemwacho sicho kikusudiwacho na msemaji. Katika hali ya namna hiyo mtafiti aligundua kuwa mbinu ya kejeli inakuwa ikitumika katika nyanja mbali mbali na kwa vipengele tofauti katika lugha ya utani inayotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Kwa mfano, katika soko la kuuzia samaki lililoko Wete mtafiti alibaini lugha hii ya kejeli ikitumiwa na wanunuzi na wauzaji wa samaki. Mathalani alitokea mvuvi mmoja akiwa na samaki wadogo wadogo akaambiwa na mchuuzi wa samaki "*Leo nahodha naona umeleta samaki wanene/ wamapande"*.

Mfano mwengine wa kejeli mtafiti aliubaini katika soko la Msuka kwa wavuvi waliokuwa wakitoka baharini kuvua samaki wakiwa na vyombo aina ya ngarawa, ambavyo vilikuwa na desturi ya kusafiri kwa kutumia matanga kupitia nishati ya upepo. Katika harakati zao za kurudi baharini walikuwa na ushindani ndani yake juu ya nani atafika mwanzo katika soko la kuuzia samaki. Kwenye safari hiyo chombo kinachotambulika kwa jina maarufu "*Tutaonana juu*" kilichokuwa mbele na ambacho ni mashuhuri kwa mbio, siku hiyo kilipitwa na chombo chengine ambacho kilikuwa si maarufu sana kinachotambulika kwa jina maarufu "*Ok na Hili kaseme*" walipofika juu lugha hii ya kejeli ilitumika kwa kuambiwa wale waliopitwa kwamba, "*Nahodha, hongera, leo nasikia badala ya tanga umefunga na mashine mbili na ukavipita vyombo vyote kama vilivyolala*".

Mtafiti kwa kuongozwa na Nadharia ya Simiotiki katika msimbo wake wa Kimatukio, ambao unalenga kuhusisha matukio mbali mbali yanayopatikana katika hadithi au kazi ya fasihi yanavyofuatana na jinsi msomaji au muhakiki anavyounda na kuelewa msuko wa kazi ya kifasihi, mtafiti alibaini kwamba kitendo cha kuambiwa nahodha wa ngarawa iliyopitwa kwamba kafunga mashine mbili na

kuvipita vyombo vingine kama vilivyolala, kauli hiyo ikuja kutokana namatumizi ya mbinu ya kejeli. Nahodha wa chombo hicho hakufunga mashine mbili kama alivyo ambiwa, na alikuwa wa mwisho kwa siku hiyo kufika sokoni hapo. Mambo kama haya tunayapata katika jamii yetu, kwani mtafiti alipokuwa akipita katika kijiji cha Konde alimshuhudia kijana akimwabia bibi yake, "*Leo bibi naona umejipura kama harusi wa kale*". Katika usemi huo kulikuwa na matumizi makubwa ya kejeli kwasababu bibi huyo hakuwa amejipura kama alivyoambiwa na mjukuu wake na badala yake alikuwa amevaa nguo chakavu.

### 4.3.6 Matumizi ya Misemo

Wamitila (2003) anaeleza kuwa misemo ni neno lenye upana na huweza kutumiwa kuelezea matamko au kauli fulani zinazoelezea ukweli fulani. Gora (2015) akimnukuu Ngure (2004) ambae anaeleza kuwa misemo ni utanzu wa Fasihi Simulizi ambao katika fani hiihutumika kisanaa. Mathalani katika uteuzi wa maneno, matumizi ya picha na uwezo wake wa kuelezea na kutathimini hali fulani tu. Fasili hii ya Ngure (ameshatajwa) inabainisha mambo muhimu yanayohusu misemo kama vile matumizi ya picha, taswira na tamathali za semi. Kwa mantiki hiyo ni dhahiri kwamba kuna matumizi mbali mbali ya misemo inayopatikana katika lugha ya utani inayotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Katika kulidhihirisha hilo tunaweza kuangalia mifano ya misemo ifuatayo: *Kijio kazi, nipa nikupe.*

Mtafiti katika data alizokusanya alifanikiwa kuisikia misemo hiyo ikitumika katika soko la kuuzia samaki lililoko Kojani. Msemo wa "*kijio kazi"* una maana ya kwamba siku zote katika maisha tunapaswa kutambua suala la utafutaji ni jambo gumu

linalohitaji maarifa na kujituma kwa hali ya juu na pasipo na kujituma si rahisi kuwepo na mafanikio katika harakati zote za kimaisha.

Msemo wa pili unaosomeka ‘’*nipa nikupe’’* una maana ya kwamba katika mazingira hayo ya masoko kunakuwa na watu wanakawaida ya kuomba samaki kwa wavuvi siku hadi siku. Katika harakati hizo za uombaji, wavuvi huutumia msemo huu wakimaanisha kwamba hawako tayari kutoa samaki wao bure na badala yake wanahitaji malipo yoyote kutoka kwa waombaji hao.

Kwa kuhusisha nadharia ya Simiotiki katika msimbo wake wa Kimatukio ambao unahusu kuhusisha matukio mbali mbali yanayopatikana katika hadithi au kazi ya fasihi yanavyofuatana na jinsi msomaji au mhakiki anavyounda na kuelewa msuko wa kazi ya kifasihi. Mtafiti aligundua watu ambao wanasifa ya kujituma kwa bidii kubwa kwa mnasaba wa kujipatia kipato chao kwa maslahi ya baadae, lakini hutokea watu na kuwabeza kwa kutumia misemo ama kweli *kijio kazi.* Watu ukiwakutia mitaani wanatanua na kujifanya wanafanya kazi maofisi makubwa makubwa ya kiserekali, lakini kumbe ukiwakutia huku masokoni wanabeba matenga ya samaki na kujipaka vumba la samaki hali ile, ama kweli *kijio kazi.* Hali kama hiyo pia hujitokeza kwenye jamii zetu, kwasababu unaweza kuwakutia watu wakifanya kazi mbali mbali kama vile kuzibua vyoo na nyenginezo, wanapata tabu wanahangaika huku na kule kwa mnasaba wa kujipatia kipato chao cha halali, lakini wanaweza kutokezea baadhi ya watu na kuwabeza kwa kazi zile wanazozifanya na kutokezea msemo kama huo ama kweli *kijio kazi*.

Kadhalika mifano mengine ya misemo mtafiti aliyofanikiwa kushuhudia ikitumika ni “*weza rohoyo na ndege mjanja*,” katika soko la kuuzia samaki lililopo Shumba ya

Mjini Kaskazini Pemba. Mtafiti kupitia data alizozikusanya alifanikiwa kuwaona waombaji wa samaki kwa wavuvi, lakini kabla ya kupewa samaki hao alitokea mtani na kumwambia yule muombaji wa samaki "*weza rohoyo"* usitafute kuadhirika watu wengine si watu wakuomba. Msemo huu unatuonesha na kutufahamisha kwamba, watu wanapokwenda kwenye masoko ya kuuzia samaki wawe na pesa za kujikimu ili wanapohitaji samaki wanunuwe kwa pesa zao, na wasipapie tu kuomba samaki wa watu kwa kila mtu wasiyemjua lakini wawaombe watu ambao wanawafahamu vya kutosha kutokana na mila na tabia za watu hao kwa kujiepusha kuaibika mbele za watu.

Mfano mwingine ni "*Ndege mjanja"*. Mfano huu unatowa maana ya kwamba katika soko hilo kuna watu maalumu ambao ni wanunuzi wa samaki lakini wana kawaaida ya kuchelewa kufika sokoni hapo kwa mantiki watu wapunguwe wakapate bei rahisi. Hata hivyo, kwa siku ile walipofika samaki wote walikuwa wamemaliza na kujikuta wanarudi watupu bila ya kupata samaki. Kutokana na sababu hiyo kulipatikana fursa ya kutumika kwa msemo huo.

Mtafiti kwa kutumia nadharia ya Simiotiki katika msimbo wake wa Kimatukio ambao moja kati ya sifa kuu na majukumu yake nikunasibisha matukio yanayotowa picha halisi ya muhusika fulani katika kazi za kifasihi, Mtafiti alibaini kwamba katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kuna baadhi ya watu ambao wanasifa na tabia kama hizo ambazo hazituletei tabia njema katika jamii. Hivyo mvuvi aliyetumia msemo wa *weza rohoyo* akikusudia kuiasa jamii na watu wengine wenye tabia ya kuombaomba katika sehemu mbali mbali kuachana na tabia hiyo, kwasababu hatima ya tabia ya kuomba omba, ni kuaibika na kufedheheka mbele za watu.

Vile vile mtafiti katika msimbo huo huo wa Kimatukio kwa kuunasibisha na msemo wa '*'Ndege njanja"*alibaini kwamba katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kuna jamii kubwa ya watu katika sehemu hizo za kazi wakiwa na tabia za uchelewaji na wanasubiri muda wa jioni wakati watu wakeshapunguwa kwa lengo la kujipatia samaki kwa bei za urahisi. Katika jamii zetu watu kama hawo wanapatikana mara kwa mara kwasababu hujitokeza baadhi ya watu wakasubiri wauzaji wa samaki (wachuuzi) muda wa jioni kwenda kununuwa samaki wakitarajia kuwapata kwa bei za urahisi, lakini mara nyengine wakisubiri muda kama huo hujikutia samaki wamemaliza na kujikutia wanakosa samaki na kula chakula kitupu. Kwa muktadha huo watu wenye sifa na tabia kama hizo jamii hutumia misemo kama hiyo kwa kuwafananisha na ndege mjanja, kwakuwa ndege mjanja hapatikana kirahisirahisi ana tabia za ujanja ujanja na wala sio rahisi kupatikana kwenye mitego iliyo madhubuti na badala yake huwa anapatikana katika mitego mibovu.

### 4.3.7 Matumizi ya majazi

Wamitila (2010) anasema kwamba majazi ni majina ambayo yana maana fulani, majina hayo yanaweza kuhusiana kitabia, maisha, matabaka, mitazamo na elimu ya muhusika. Kutokana na dhana hiyo tunaweza kusema majazi ni mbinu ya kumpa mtu jina linaloakisi au kuelekeza kwenye wasifu wa tabia zake. Mtafiti amegundua mbinu hii ya majazi ikitumika katika lugha ya utani inayotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kama sehemu ya utani wao. Mfano ufuatao unathibitisha:

Katika soko la kuuzia samaki lililopo Tumbe kuna matendo ya watu kuitana majina *"jembe", "janga", "kishindo"*na majina mengine kama hayo. Mtafiti ameyatafsiri

majina haya kama ni matumizi ya majazi. Jina *"jembe"* kwa kawaida tunalifahamu ni kifaa kinachotumika kwa watu kulimia shambani, lakini kwa mazingira ya sehemu hiyo limetumika kuitwa mtu kulingana na tabia zake za kuchukuwa samaki wa watu bila ya huruma. Vile vile jina *"janga"* katika hali ya kawaida ya tafsiri ya vijijini lina maana ya mtu mwenye kutumia tabia za kichawi, lakini kwa mazingira ya sehemu hizo jina hili linatumika kutokana na tabia za mtu ambae anaweza kuwachukuwa samaki wa watu kwa mazingira yale anayotaka mwenyewe bila ya watu kujua. Hata hivyo jina *"kishindo"* linatumika kutokana na tabia za mtu ambapo mara kwa mara katika matendo yake huwa anatumia vishindo.

Mbinu hii ya majazi pia mtafiti aliibaini kutumika katika soko la kuuzia samaki lililoko Msuka. Katika shughuli za ukusanyaji wa data mtafiti aligunduwa kuwa yuko mnunuzi mmoja wa samaki ambae anaitwa *"Ngogo"* jina hili katika mazingira ya masokoni hujuilikana kama aina ya samaki ambae anapatikana baharini. Wasifu wa samaki huyu ni mweusi na mwenye miba mikali sana ambayo ikimchoma mtu anapata machungu makali sana ambayo yanaweza kumsababishia homa. Hata hivyo, jina hili katika mazingira ya utani linatumika kwa kunasibishwa na mtu ambae ni mnunuzi wa samaki kwa sababu bei zake ni ghali ambazo akizitowa watu zinawachoma moyoni mithili ya miba ya *ngogo*. Mnunzi huyu ni mchuuzi ambaye huuza samaki kwa watu wa kawaida mitaani baada ya kuwanunua sokoni.

### 4.3.8 Matumizi ya Methali

Methali ni semi au sehemu ya lugha ambayo hufananishwa na kiungo cha lugha au kitoweo cha lugha. Aidha methali hutumiwa kwa kutafakari na kupima maisha, kufunzia jamii kulingana na mazingira ya binadamu (Senkoro, 1982). Kwa mantiki

hiyo kuwepo kwa methali katika maisha ya binadamu tunaweza kusema ni utajirisho wa fani na maudhui katika kazi ya kifasihi. Katika utafiti huu mtafiti alishuhudia baadhi ya methali zikitumika katika lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba kama vile *"Mgagaa na upwa, hali wali mkavu"*. Methali hii inatufahamisha kwamba mtu ambae ni mtafutaji wa kitu si sawa sawa na mtu ambae amekaa tu bila ya shughuli yoyote.

Mfano mwengine wa methali ambao mtafiti ilibaini ikitumika ni "*Kila chombo na wimbi lake*" *na* "*Ukiona vyaelea jua vimeundwa*". Mtafiti mara baada ya kuzichunguza methali hizi jinsi zilivyozikitumika katika soko hilo amebaini kwamba mfano huo wa methali, *kila chombo na wimbi lake* ulionesha tofauti ya uwezo uliopo baina ya wanunuzi wa samaki. Mtafiti akiwa sokoni hapo alishuhudia samaki wakubwa aina ya *Jodari,* ambao walikuwa na bei kubwa, wanunuzi wa vijijini waliposogelea samaki hao, wanunuzi wa mjini ambao wanaonekana na uwezo wa hali ya juu walitumia methali hiyo wakimaanisha kwamba watu wa vijijini hawana uwezo wa kununuwa samaki aina ya jodari.

### 4.3.9 Matumizi ya tashititi

Miongoni mwa mbinu za kisanaa zilizojitokeza katika kazi hii ni tashititi. Kwa kawaida msanii huitumia mbinu hii kuuliza maswali ambayo anayajua majibu yake katika kazi ya fasihi. Mtafiti baada ya kuchunguza na kuchambua lugha ya utani inayotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba amebaini mbinu hii ya kisanaa inatumika. Mfano ufuatao unadhihirisha ukweli huu:

Katika soko la kuuzia samaki lililopo Tumbe, mtafiti wakati wa kukusanya data alimuona samaki mkubwa aina ya *"pungu,"* samaki huyo aliuzwa kwa bei kubwa na

muuzaji wa samaki. Mtu aliyenunuwa samaki huyo ni mnunuzi wa kawaida ambae ana kawaida ya kununua jamii ya samaki huyo siku zote pindi akipatikana. Lakini mara baada ya muda mfupi kupita baada ya mauzo ya samaki huyo, mtafiti alimshuhudia muuzaji wa samaki maarufu akimuuliza yule mnunuzi wa samaki "umemuona yule samaki uliyenunua alivyokuwa rahisi?" Muulizaji anauliza swali wakati anajuwa fika samaki huyo alikuwa na bei ya juu.

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki katika msimbo wake wa kimatukio ambao moja katika wajibu na majukumu yake ni kuhusiana na matukio jinsi yanavyopatikana katika hadithi na namna yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuelewa msuko wa kazi ya fasihi. Mtafiti alibaini kwamba baadhi ya lugha za utani za tashititi zinazotumika katika masoko ya kuuzia samaki hazioneshi bezo wala kero, bali ni moja kati ya mila na desturi zinazotumika katika sehemu hizo kwa mnasaba wa kukuza mahusiano mema miongoni mwa wanajamii.

**Jadweli namba 04: Muhutasari wa mbinu za kisanaa za lugha ya utani**

| **Nambari** | **Mbinu za Kisanaa za Lugha ya Utani** | **Maelezo** |
|---|---|---|
| i) | Matumizi ya Tashbiha | √ |
| ii) | Matumizi ya Taswira | √ |
| iii) | Matumizi ya Takriri | √ |
| iv) | Matumizi ya Ishara | √ |
| v) | Matumizi ya Kejeli | √ |
| vi) | Matumizi ya Misemo | √ |
| vii) | Matumizi ya Majazi | √ |
| viii) | Matumizi ya Methali | √ |
| ix) | Matumizi ya Tashtiti | √ |
| | **Jumla** | **9** |

(Chanzo: mtafiti 2023)

## 4.4 Hitimisho

Sura hii imeweza kutekeleza na kutimiza malengo mahususi ya utafiti kwa kuwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti zilizohusiana na dhamira na mbinu za kisanaa katika lugha ya utani inayotumika kwenye masoko ya samaki kisiwani Pemba. Kwa jumla imebainika kwamba, utani katika masoko hayo huibua dhamira zenye malengo mazuri katika jamii ikiwa ni pamoja na upendo, kuhimiza uwajibikaji katika kazi, kuonya jamii na kuburudisha kutaja kwa uchache. Pia, utani una matumizi ya mbinu za kisanaa kama vile matumizi ya tashibiha, taswira, ishara, misemo, methali na tashititi kutaja kwa uchache.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ya mwisho inahusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Utafiti uliongozwa na malengo mahususi mawili ambayo yametimizwa kikamilifu katika sura ya nne ya tasnifu hii. Muhtasari wa matokeo ya utafiti ni kama ifuatavyo:

## 5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulidhamiria *kuchunguza dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba.* Matokeo ya utafiti yamebainisha aina za utani unatumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba ambazo ni utani wa kimatendo, utani wa kimisemo na utani wa majina. Vile vile utafiti huu umechambua dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba, pamoja na kubainisha mbinu za kisanaa za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba.

Lengo la kwanza lilikuwa ni kuchambua dhamira za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Lengo hili liliongozwa na swali lisemalo kwamba, ni dhamira gani za lugha za utani zimejitokeza katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba? Katika kulijibu swali hili, matokeo ya utafiti yamebaini kuwepo dhamira kadhaa ambazo ni kujenga umoja na mashirikiano, kuelimisha jamii, kuburudisha jamii, ustahamilivu katika kazi, kujenga ujasiri, ukakamavu katika kazi, kuhimiza jamii katika kazi, kuwa na upendo katika kazi, kuonya jamii, mmong'onyoko wa maadili, utamaduni katika jamii, ukombozi na ukweli na uwazi.

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha mbinu za kisanaa za lugha ya utani katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba. Lengo hili liliongozwa na swali ni mbinu zipi za kisanaa za lugha za utani zimebainishwa katika masoko ya kuuzia Kaskazini Pemba? Katika kulijibu swali hili, matokeo ya utafiti yamebaini kujitokeza kwa mbinu anuwai za kisanaa katika utani wa jamii ya Wapemba wa masoko ya samaki. Mbinu hizo za kisanaa ni pamoja na matumizi ya tashbiha, taswira, takriri, ishara, kejeli, misemo, majazi, methali na tashtiti.

## 5.3 Hitimisho

Baada ya kufanyika kwa utafiti huu, matokeo ya utafiti yamebainisha kwamba utani unaotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba unafaa na ni hazina kubwa katika kutunza mila na desturi za Wapemba. Utani pia huibua dhamira mbali mbali zinazoweza kutumika katika jamii ya leo kwa lengo la kukuza maadili na uwajibikaji kwa vijana ambao ndiyo muhimili na nguvu kazi ya taifa.

## 5.4 Mapendekezo

Tunapendekeza kufanyika kwa tafiti nyengine katika sehemu mbali mbali za Zanzibar na Tanzania kwa jumla ili kuibainisha umuhimu wa utani katika jamii mbali mbali kwa mawanda mapana zaidi. Utafiti zaidi ufanyike katika kipera cha utani ambacho ni mojawapo kati ya vipera vya utanzu wa sanaa za maonesho.

### 5.4.1 Mapendekezo kwa Jamii

Jamii mbali mbali za Kizanzibari zinashauriwa kuenzi utani na kuuendeleza kwasababu utani ni kipengele kimoja wapo miongoni mwa vipengele vya kiutamaduni kilicho na umuhimu mkubwa kwa Wazanzibari husasani kwa watu wa

jamii ya Kipemba. Utani unatoa ujumbe unaoakisi hali halisi ya maisha ya watu na harakati zao za kila siku. Aidha, wazazi wanashauriwa kuwafahamisha watoto wao kuwa utani ni sehemu ya utamaduni wa Kizanzibari. Hivyo wanapaswa kuuenzi na kuacha hulka za kupenda na kuiga tamaduni za kigeni.

## MAREJELEO

Abdalla, A. (2018). *Dhamira na Fani Katika Nyimbo za Taarab Asilia*. Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Abourweeshah, A. (2017). *Matumizi ya Mbinu za Kisanaa na Dhamira katika Tamthilia ya Morani.* Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, Nairobi: Oxford University.

Barthes, R. (1994). *The Semiotic Challenge Berkley*. Califonia: University of Calfonia Press.

Bogdan, R. & Biklen, S. K. (1992). *Qualitative Research of Educatin: An Introduction to Theory and Methods (Edrs),* Boston: Allyn and Bacon.

Bryman, A. (2004). *Social research methods (2nd edition).* London: Oxford University Press.

Cooper, R. (1989). *Language planning and social change.* Cambridge: Cambridge University Press.

Cresswell, J. W. (2009). *Research design qualitative, quantitative and mixed method approach.* Los Angels: SAGE Publication.

De Saussure, F. (1966) *A course in general linguistics*. (W. Baskin, Trasns) New York: Mc Graw Hill.

Enon, D. C. (1998). *Research, statistics and measurements.* Makerere: Makerere University press.

Freeman, J. (1977). *Joking, affinity and the exchange of vitual services among the Kiga of Northern Rwanda:* An essay on joking realationship theory. Man 12(1) 154-65.

Gora, S. (2015). *Utani katika sherehe zaa harusi za Watumbatu: Aina, sababu na taashira zake*. Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Haji, Z. (2017). *Kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto: Mifano kutoka Makunduchi.* Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya fasihi linganishi, nadharia, mbinu na matumizi*. Dar-es Salaam: Daud Publishers.

Kiesling, S. F. (1997). *Power and the language of men.* In S. Johson and U. H. Meinhof (eds), language and masculinity, Oxford: Blackwell.

Kombo, D. K. & Tromp, D. L. (2006). *Proposal and thesis writing: An introduction*. Nairobi: Paulines Publications.

Kothari, C. R. (2003). *Research methodology: methods and Techiniques. 2nd ed*. New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Kothari, C. R. (2004).*Research methology*: *Methods and techniques*. New Delhi: New Age International Publishers.

Kothari, C. R. (2008). *Research methodology*: *Methods and techinques*. New Delhi: New Age International Publisher Ltd.

Kothari, C. R. (2013). *Reearch Methodology: Methods and techniques*. 2nd ed, New Delhi: New Age International Publisher Ltd.

Kouyate, S. (2003). *Le cousinage a plaisanterie*. Conakry: Notre Heritage Commun.

Kuranchie, A. (2012). *Student's nick names: Their source and effects on Learning*. Accrah: Catholic University College of Ghana.

Liao, C. C. (2006). *Linguistic analysis of nicknames of junior high school students*. Kaohsing: Taiwan National University of Kaohsing.

Massoud, R. (2018). *Tathmini ya maana na vigezo vilivyotumika kutoa Majina ya utani kwa jamii ya Wapemba.* Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Tanzania (Haijachapishwa).

Mc Connell, Ginet, S. (2005). *What's in a names social labeling? In Janet Holmes and Miriam.* London.

Mehrabian, A. & Piercy M. (1993). *Differences in positive and negative Connotations of nicknames and given names*. Journal of Psychology.

Mgakazi, M. (2010). *The Basuta jokes*. Dar es Salaam: Aera Kiswahili Researched Products.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya hadithi fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa fasihi*.Nairobi: EAEP Ltd.

Mzandi, M. M. (2011). *Nafasi ya utani wa msibani na harusini katika kabila la Wadigo*. Utafiti katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ngure, A. (2003). *Fasihi simulizi*. Nairobi: Phonex Publishers.

Ngure, A. (2005). *Fasihi simulizi kwa shule za sekondari*. Nairobi: Phonex Publishers.

Njogu, K. & Wafula. R. M. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Newman, W. L. & wenzake, (2006). *Social research.* $6^{th}$ ed. Boston: Person

Omary, I. M. (2011). *Education research concept and methods*. Dar es Salaam: Delah Educational Publisher Ltd.

Opie, C. (2004). *Doring education research.* New York: SAGE Publicatin Ltd.

Orodho, A. J. (2003). *Essentials of education and social science research methods*. Naorobi: Masola Publisher.

Panneerselvan, R. (2004). *Research methodology*. New Delhi: Learning Private Limited.

Ponera, A. S. (2010). *Ufutuhi katika nathari za Shaaban Robert: Maana yake, sababu za kutumiwa, na athari zake kwa wasomaji.* Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Rashid, O. Z. (2011). *Athari ya lugha ya utani kwa jamii ya Wapemba wa Zanzibar*. Tasinifu ya umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Cha Kiislamu Uganda.

Sengo, T.Y .S. M. & Lucas, S. (1975). *Utani na jamii ya Ukerewe.* Nairobi: *Foundation Books Ltd*.

Sengo, T. S. Y. (2009). *Sengo na fasihi za kinchi.* Dar es Salaam: Al-amin Education and Research Academy.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*, Dar es Salaam: Kampuni ya utamaduni, tafsiri na uchapishaji.

Shankle, G. E. (1995). *American Nicknames: Their origin and significance*. (2nd Ed). New York: The H.W.Wilson Company.

Suta, D. D. & Mnyamba, F. A. (1999). *A Case of Reproduction and Articulation of Utani Umong the Bena Ethic Group in Tanzania.*

TUKI (1990). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi, misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha fasihi simulizi na andishi*. Mombasa: Focus Publisher Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa

Wamitila, K. W. (2010). *Kichocheo cha fasihi* simulizi na andishi. Nairobi: Focus Books.

Waziri, F. M. & Dlourine, F. M. (1998). *The case of reproduction and articulation of utani among the Pare of Tanzania*.

Zaid, O. R. (2011). *Athari za lugha ya utani katika jamii ya Wapemba*. Tasnifu ya Umahiri ya Chuo Kikuu cha Kiislamu Uganda.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO 1

## MWONGOZO WA MASWALI YA UTAFITI KWA WATAFITIWA

1. Unafahamu / unaujuwa nini kuhusu Utani?

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

2. Unafikiri / unadhani ni lipi lengo kuu hasa la Utani?

   ………………………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………....................

3. Je, wewe umeshawahi kutaniwa au kutania?

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

4. Je, Mnapotaniana huwa mnafurahi au mnachukia?

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

5. Kuna ujumbe wowote unaopatikana katika Utani huo?

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

6. Je, unaweza kunitajia Utani wowote unaotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba?

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

7. Ni kwanini mnataniana katika masoko ya kuuzia samaki?

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

8. Naomba unitajie aina za Utani ambao mnataniana?

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

9. Je, kuna sababu au dhamira zozote zinazopatikana katika Utani huo hapo sokoni?

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

10. Unafikiri lugha ya utani inayotumika katika masoko ya kuuzia samaki Kaskazini Pemba inatumia ufundi gani wa kisanaa katika maisha ya kila siku?

………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

11. Utani unaotumika sokoni kwa kuuzia samaki unaendana vipi na mila na utamaduni hasa wa Wapemba?

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

## KIAMBATANISHO II

## JADWELI 02. MUHTASARI WA AINA ZA LUGHA YA UTANI KATIKA MASOKO YA KUUZIA SAMAKI KASKAZINI PEMBA

| | | |
|---|---|---|
| Kusukumana | Kama umvuvi tutaonana mwambani | Ngisi |
| Kupigana | Tutaonana juu | Pweza |
| Kulipiwa mtu samaki na kuambiwa achukuwe bure | Chukuwa ukampe mke wetu | Fatuma |
| Kutiana matope | Haigwi | Tobwe |
| Kurushia maji ya vumba | Goyalyo | Wamapande |
| Kutia samaki mchanga na mwenyewe kuwafuta. | Matului (hayumo katika watakao uzwa) | Bwege |
| Kukonyezana | Nyegezo | Jembe |
| Kuoshwa miguu | Sukuma twende | Kishindo |
| Kununuliwa samaki | Kale na mkeo | Nahodha |
| Kutia mchanga samaki | Kampe mke wetu | Kidege |
| Kushikwa matako | Bwege | Tajiri |
| Kushikana mashavu | Mshenzi | Bosi |
| Kushikana chuchu | Khanithi | Mzee |
| Kutukanana | Nipe nikupe | Mjinga |
| Kufichiana samaki | Msenge | Janga |
| Kutia bei kwa ajili ya kukomoana | Mwehu | Mchachuo |
| | Mwendawazimu | Datuu |
| | Kijiokazi | Ngogo |
| | Tope | Pono |
| | | Ng’ombe wa Pwani |
| | | Pepe kale |
| | | Papa/ Mbuyu |
| | | Tope |

# KIAMBATANISHO III

## ORODHA YA PICHA MBALIMBALI ZINAZOONYESHA KATIKA MASOKO YA KUUZIA SAMAKI KASKAZINI PEMBA



**Picha Nambari 01:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akiwa katika soko la kuuzia samaki Msuka Wilaya ya Micheweni Kaskazini Pemba akifanya mahojiano na wavuvi na wanunuzi wa samaki sokoni hapo. (Utafiti, Oktoba 2019)



**Picha Nambari 02:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akifanya mahojiano na mnunuzi wa samaki katika soko la kuuzia samaki Wete katika Wilaya ya Wete Kaskazini Pemba. (Utafiti, Oktoba 2019)



**Picha Nambari 03:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akifanya mahojiano na wanunuzi wa samaki katika soko la samaki la Tumbe. (Utafiti, Oktoba 2019)



**Picha Nambari 04:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akifanya mahojiano na Mzee Ali Hamadi Shante (Mzee wa soko) katika soko la Kojani. (Utafiti, Oktoba 2019)



**Picha Nambari 05:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akifanya mahojiano na mvuvi na ambae ni nahodha (kiongozi) katika Soko la Tumbe. (Utafiti, Oktoba 2019)



**Picha Nambari 06:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akifanya mahojiano na mvuvi Hamad Mawana (Nyedi) ambae pia ni nahodha wa chombo aina ya mashua wakiwa ndani ya maji ya bahari katika Soko la Kojani. (Utafiti, Oktoba 2019)




**Picha Nambari 07:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akifanya mahojiano na wanunuzi wa samaki katika soko la Msuka. (Utafiti, Oktoba 2019)



**Picha Nambari 08:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akifanya mahojiano na mnunuzi wa Samaki katika Soko la Wete. (Utafiti, Oktoba 2019)



**Picha Nambari 09:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akiwa kati kati ya wanunuzi wa Samaki akishuhudia ununuzi wa samaki katika soko lililoko Shumba ya Mjini wakati wa kukushanya data. (Utafiti, Oktoba 2019)



**Picha Nambari 10:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akifanya mahojiano na mnadishaji wa samaki (dalali) katika Soko la Shumba ya Mjini. (Utafiti, Oktoba 2019)



**Picha Nambari 11:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akifanya mahojiano na mmoja kati ya wazee katika Soko la Wete. (Utafiti, Oktoba 2019)




**Picha Nambari 12:** Mtafiti (aliyevaa shati ya manjano) akifanya mahojiano na mvuvi katika Soko la Tumbe. (Utafiti, Oktoba 2019)




**Picha Nambari 13:** Ramani inayoonesha kisiwa cha Pemba (Utafiti, Oktoba 2019)